# NDOA YA KIISLAM

H.H. MBYANA

## UTANGULIZI

JAMAA wengi walitaka tuandike kitabu kielezacho habari za Ndoa na mambo mengine yanayohusu ndoa kwa kufuata Sheria ya Kiislamu na maagizo ya Mtume wetu Muhammad s.a.w. Ijapokuwa makala nyingi nzuri sana zilipigwa chapa juu ya makala hii katika matoleo mbali mbali ya Gazeti la Mapenzi ya Mungu katika miaka iliyopita; lakini tumeona vizuri kuitengeneza makala hii katika sura ya kijitabu ili kutimiza haja mbali mbali na kuwa majibu ya maswali mbali mbali yanayoulizwa mara kwa mara na ndugu zetu Waislamu hata Wakristo.

Tuna yakini makala hii itawafaa jamaa hawa wote na itakuwa sababu kubwa ya kuwaongoza kwenye maisha mema ya nyumbani ambayo msingi wake hasa ni ndoa.
Mwalimu Hemedi Mbyana ameandika makala hii.

Ahmadiyya Mosque.
Fort Hall Road.
P.O. Box 40554.
Nairobi.

**SHEIKH NUR-EL-HAQ ANWAR**
**Mbashiri wa Islam**

# YALIYOMO


UTANGULIZI ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ii

MWONGOZO .. ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 1

NDOA ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 4

FAIDA YA NDOA .. ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 4

NDOA HUFUNGWA KWA NJIA GANI ... ... ... ... ... ... ... 5

KUCHAGUA MCHUMBA: ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 6

KUMWOMBA MWENYEZI MUNGU ... ... ... ... ... ... ... ... 7

KUFUNGA NDOA ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 10

WALIMA ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 12

KIWANGO CHA MAHARI ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 15

MKE NA MUME WANA WAJIBU GANI? ... ... ... ... ... ... 17

WANAWAKE WALIO HARAMU KUWAOA ... ... ... ... ... 21

HARAMU KUFUNGA NDOA NA WASHIRIKINA ... ... ... 23

KUOA ZAIDI YA MKE MMOJA ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 24

TALAKA ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 27

KUPATANISHWA WAGOMBANAO ... ... ... ... ... ... ... ... 28

JINSI YA KUACHANA ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 29

MAMBO MENGINE YA MWONGOZO ... ... ... ... ... ... ... 32

MAAGIZO MEMA KWA WANAWAKE: ... ... ... ... ... ... 34

## MWONGOZO

1. Kaka ninakusalimu
Salamu alaykum,
Roho yangu yanihim,
Nikweleze ya murua.

2. Kaa ukizingatia,
Dunia yakukimbia
Kila unapopumua
Umri wakupungua

3. Basi ufikiri sana
Jambo lipi lenye mana,
Ambalo kwa subuhana
Utaja liwasilia

4. Nakusihi unyamaze
kwanza unisikilize,
Uyapime uyawaze
Yote nitayo kwambia

5. Mwenyezi kakufadhili
Kakupa njema akili
Kisha amekupa mali
Ufurahie dunia

6. Amekupa na wasaa
Pote upendapo kaa,
Ardhi ametandaa,
Upate kuitumia

7. Na vingi vitu vizuri
Vilo na nyingi ghururi
ameviweka tayari,
Ili kukujaribia

8. Na hivyo ndio ulufu
Amevijaza Latifu
Mwenyezi Mkamilifu
Akhi kweli nakwambia

9. Akaweka na mipaka,
Kaka upate ishika
Na hiyo ukiiruka
Motoni utaingia

10. Huo ndio mtihani
Aliokupa Manani
Kuukwepa asilani
Huwezi kupata njia

11. Nadhani huwezi kana,
Nikikwambia bayana,
Mfano wa wasichana
Ambao wakuzengea

12. Mtihani huu kaka,
Ni mgumu kwa hakika
Walimwengu kadhalika
Wengi wana ujutia.

13. Lakini Mwenyezi Mungu
Aliyeziumba Mbingu,
Amewapa walimwengu
Kitu cha kuwaongoa

14. Kitu hicho ni funguo,
Ifunguayo mioyo,
Jitahidi uwe nayo,
Njia itajifungua.

15. Kitu hicho sikuhini
Ni Kitabu Kuruani
Alichoshusha Manani
Kuwaongoa insia

16. Kitabu hicho chanena
Amri za Maulana
na yote aliyokana
Viumbe kutotumia

17. Basi katika Kurani,
Mwenyezi Mungu Manani
Amekana “Usizini”
Hilo jambo la hatia

18. Pia ametoa njia,
Ambayo nakutakia
Kaka yangu nawe pia
sana kuishikilia

19. Ya kwamba “uoe” mke
Wewe na yeye wa peke
Mpendane na mcheke
mfurahie dunia

20. Na huo ndio mpaka,
Alioweka Rabuka
Upate kunusurika
Na ghururi za dunia

21. Ufahamiwe uzinzi
Ndilo jambo lenye manzi
Walo uzamia mbizi
Kesho watakuja lia

23. Basi tafadhali wahi,
Akhi ufunge nikahi,
Ndio suna yake Mahi
Mtume wetu Nabia

24. Tumwa wetu Muhammadi
Safari moja kanadi
Kufunga ndoa ni budi
Juu ya kila insia

25. Mtu asotaka oa
Muhammad katongoa
Huyo amesha jitoa
Katika yangu jamia

26. Kaka hebu tafadhali
Weka katika akili
Mwenyezi Wake Rasuli
Hayo ameshatongoa

27. Unakumbuka Ghulam
Kwamba Nabii Adamu
Adeni kasitakim
Pamoja na Bibi Hawa.

28. Hao watu wa azali
Walokuwa na qibali
Mbele ya Dhul Jalali
Nao walifunga ndoa

29. Utazame Ulimwengu
Uli na mingi  mizungua
Usije kukaza pingu
Ushindwe kuzifungua

30. Haya ninayo kwambia,
Mwenyewe wayatambua
Si ghali kama halua
Yaoneka dhahiria

31. Watazame wanawali,
Wenye rangi za kipali
Jinsi wanavyokabili
Uchi kujitembelea

32. Wanafika majumbani,
Hodi kaka Selemani
Siku hizi sikuoni
Wapi unatembelea.

33. Kaka siku nyingi sana,
Tangu nilipokuona,
Moyoni mwangu naona
Kukukosa ni udhia.

34. Hiyo ndiyo mitihani,
Nami nakupa ilani,
Ya kweli na si utani
Ndoa ndio yake njia.

35. Basi ndugu pulikiza,
Mpate bibi Aziza
Ambaye kakupendeza
Kwa umbo na kwa tabia.

36. Fika kwa wazazi wake,
na mahari uiweke
Uwaombe waridhike
Aziza kumchukua,

37. Kisha msome sheria
Alizotoa jalia
Zenye kuongoza njia
Njia ya kumfikia.

38. Kuruani Takatifu
Kitabu chake Latifu
Kakupeni ya unyofu
Mpate kusitawia

39. Na hiki kitabu changu,
Nimemegua vifungu
Alivyovitoa Mungu,
Kwenye maisha ya ndoa.

40. Nakuombea kwa Mungu,
Ewe mpenzi kakangu,
Katika hivyo vifungu,
Uweze kupata njia.

**H. H. Mbyana.**

## NDOA

“Enyi watu!. mcheni Mola wenu ambaye Amewaumbeni katika nafsi moja, na Ameumba katika nafsi ile mwenziwe, na Akaeneza kutoka hao wawili wanaume wengi na wanawake; na Mcheni Mwenyezi Mungu Ambaye Kwake mnaombana na (kuangalia) jamaa wa damu; hakika Mwenyezi Mungu ni Mlinzi juu yenu”. (Sura 4 Aya 2).

Aya hii inaeleza kuwa kwa njia ya mke na mume ndio kizazi kinaweza kuendelea na ujamaa wa damu unapatikana. “Ameumba katika nafsi ile mwenziwe. Na Akaeneza kutoka hao wawili wanaume wengi na wanawake”. Ndio kusema ya kwamba kufanya ndoa na kuendeleza kizazi ni amri ya Mwenyezi Mungu, na mtu asiyetaka kabisa kufanya jambo hili amevunja amri ya Mwenyezi Mungu na makusudio yake.

## FAIDA YA NDOA

Faida kubwa kabisa ya kufunga ndoa ni kukuza taifa. Mafanikio ya taifa, nguvu yake na ustawi wake sana sana yanategemea juu ya wingi wa watu wa taifa lenyewe.
Taifa lenye watu kidogo halina ila kupotea ndani ya taifa jingine kubwa au kuishi katika hali ya unyonge milele. Taifa linalotafuta kupunguza hesabu ya watu wao au linalojaribu kuzuia wasizaliane sana watu, taifa hilo linajichimbia Ienyewe shimo la kuangamia kwake. Wingi ni nguvu kubwa katika maisha ya kilimwengu na ni vigumu kabisa kuwazuia wengi. Nzige ni wadudu tu tena wadogo lakini kwa sababu ya wingi wao wakulima wote wanataharaki. Sisimizi juu ya udogo wao, wanapokusanyika, mende na ukubwa wake, kama hakukaa

vema, atakokotwa akitaka asitake. Hivyo ni rahisi kuona ya kwamba wingi wa watu ni sehemu kubwa kabisa ya nguvu yao.

Bara la Afrika ni kubwa kabisa kuliko Ulaya, lakini watu wa Ulaya ni wengi zaidi kuliko Waafrika. Imekuwa tabia katika nchi zenye watu wengi sana kuhama watu wao na kwenda fanya maskani zao katika nchi zingine, na kwa njia hii wakapanua taifa lao, milki na nguvu yao. Basi taifa kama la Waafrika hasa katika siku hizi hapana budi kama tukitaka tulipe nguvu na haiba mbele ya ulimwengu ni lazima tushike njia ya kuoa ili wazaliwao wawe na afya njema na baraka kwa ajili ya manufaa ya kesho. Watu wanaofikiri kuwa hawana haja ya kuoa, bali wafanye kazi ya uzinzi tu kuharibu heshima ya taifa lao, hao ni maadui kabisa wa taifa wanahesabiwa kuwa ni wafisadi katika ufalme wa Mwenyezi Mungu.

“Mtu aliyeoa amekamilisha nusu nzima ya dini yake” (Muslim). Kuoa ni msingi wa mtu kuacha maovu mengine. Na kwa sababu hii Mtume s.a.w.; akasema kuwa nusu nzima ya dini ya mtu imo katika kufunga ndoa. Basi hapa chini, wasomaji wetu, nitakuelezeni kanuni na sheria za ndoa kama zilivyowekwa na Mwenyezi Mungu na Mtume wake s.a.w.

## NDOA HUFUNGWA KWA NJIA GANI

Kabla ya kueleza jinsi ndoa inavyofungwa, ningependa kuwafahamisheni kuwa dini ya Islam inazifahamu ndoa zinazofungwa kwa njia ya dini zingine kuwa pia ni ndoa za halali. Kama Wakristo wawili mume na mke waingie katika Dini ya Islam hawana haja ya kufunga ndoa upya. Lakini ingawa Dini ya Islam inazifahamu ndoa za dini zingine kuwa

ni za halali, imeweka, kanuni na sheria ya ndoa kwa namna kamilifu kabisa inayopatana na kuhusiana na watu wa hali zote na wa nyakati zote.

Katika Dini ya Islam ndoa haiwi bila ya idhini ya binti mwenyewe anayetaka kuolewa na pia idhini ya wazazi wake endapo binti huyo ni bikira asiyepata bado kufahamu na kuyajaribu maisha ya ndoa. Idhini ya wazazi humsaidia msichana kwa njia nyingi. Wazazi kwa kuwa wao wanafahamu mengi zaidi na wenyewe wameishi maisha hayo ya ndoa wanaweza kumsaidia binti wao kwa kumpatia mume mwenye tabia na mwenendo mzuri. Pengine hinti kwa kumwona tu mchumba wake anaanza kumwona ni mzuri na kusema kuwa anamkubali pasipo kufahamu zaidi juu ya tabia na mwenendo wake. Na hii humletea taabu mara aishapo kuolewa. Kwa sababu hii Dini ya Islam imeweka kanuni ya kwamba ndoa isifungwe bila ya idhini ya wazazi.
Mtume s.a.w. alisema. “Hakuna ndoa bila idhini ya mlinzi” (Ibn Majah).

## KUCHAGUA MCHUMBA:

Kabla ya mtu kuoa ni lazima afikiri kwanza atamwoa nani. Je. atamwoa kwa sababu ni mzuri wa sura au umbo na kumbe tabia si njema? Au atamwoa kwa sababu ni mwanamke wa nyumba kubwa? Basi Mtume wetu Muhammad s.a.w. ametoa mwongozo akasema:-
“Mwanamke anaolewa kwa mambo manne: (1) kwa sababu ya mali yake. (2) kwa sababu ya utukufu wa ukoo wake. (3) kwa sababu ya uzuri wake na (4) kwa sababu ya tabia yake

nzuri na dini yake. Basi jipatie ufaulu kwa kumpata yule mwenye tabia nzuri” (Bukhari).

Hii ndiyo hekima iliyo ghali sana kupatikana. Watu Wengi hawajui siri hii. Kusema kweli maisha yenye raha na mafanikio yanategemea mke mwenye tabia njema na mwenendo wa murua. Bila ya hayo, kama mtu hakuangalia anaweza kumaliza wanawake chungu nzima na asipate raha.

Basi njia bora ni hi tu aliyofundisha Mtume s.a.w. ya kwamba tuwapate wanawake wenye tabia njema ambao wanaweza kuwa mama za watoto wema na hata watoto wetu wapate mafunzo mema kwao, na sisi tupate raha, furaha na starehe.

Mtu anayo ruhusa kumwona mchumba wake.

Mtume s.a.w. akasema:-

“Mmoja wenu anapotaka kumchumbia mwanamke, basi atazame kile kinachomvuta kwake” (Abu Dawud).

“Mwanamke ana ruhusa kumtazama mchumba wake, kwa maana cho chote kitakachompendeza kwake kitampendeza mwanamume vile vile kwake yeye, na kila mmoja wao anaweza kumtazama mwenziwe ili alama zote zionekane wasije wakajutiana baada ya ndoa”.

Kwa Hadithi hizi za Mtume s.a.w. Dini ya Islam inafundisha kuwa ni shauri bora wachumbianao watazamane kabla ya kukata shauri. Na hivi inafaa zaidi wapewe muda kidogo wa kufikiri tena kabla ya kufunga ndoa.

## KUMWOMBA MWENYEZI MUNGU

Kuna watu wenye bahati kubwa waliopata, kwa ajili ya utakatifu na utawa wao, kufikia ukaribu sana na Mwenyezi Mungu hata inakuwa ya kwamba wanapofikiwa na Mambo ya namna hii, kabla ya kufanya lolote kwanza humwomba Mungu Mwenyezi awafunulie matokeo yake, nao wengi wakapata mwongozo kwa Yeye Aliye ndiye Mjuzi wa wajuzi. Na njia hii basi ndiyo bora kabisa ninayowashauri wasomaji wapenzi mwishike. Kwani shauri la Mwenyezi Mungu huwa la mwisho katika mambo yote. Kama wawe wazazi wa msichana au msichana mwenyewe au mwanamke mzima au mvulana mwenye kuchumbia, hili litakuwa jambo jema kulishika kuliko yote. Mtume Muhammad s.a.w. mwenyewe alikuwa akiomba dua juu ya mambo ya namna hii. Kabla ya kwenda kulala, baada ya Sala ya Isha alitawadha vizuri na akasali rakaa mbili, na katika Tahiyyatu aliomba dua hii:-

اَللّٰهُمَّ اِنِّیۤ اَسْتَخِيْرُكَ بِعِلْمِكَ وَاَسْتَقْدِرُكَ بِقُدْرَتِكَ
وَاَسْئَلُكَ مِنْ فَضْلِكَ الْعَظِيْمِ فَاِنَّكَ تَقْدِرُ وَلَا اَقْدِرُ وَتَعْلَمُ
وَلَا اَعْلَمُ وَاَنْتَ عَلَّامُ الْغُيُوْبِ ـ اَللّٰهُمَّ اِنْ كُنْتَ تَعْلَمُ اَنَّ
هٰذَا الْاَمْرَ خَيْرٌ لِّیْ فِیْ دِيْنِیْ وَمَعَاشِیْ وَعَاقِبَةِ اَمْرِیْ فَاقْدِرْهُ
لِیْ وَيَسِّرْهُ لِیْ ثُمَّ بَارِكْ لِیْ فِيْهِ وَاِنْ كُنْتَ تَعْلَمُ اَنَّ هٰذَا
الْاَمْرَ شَرٌّ لِّیْ فِیْ دِيْنِیْ وَمَعَاشِیْ وَعَاقِبَةِ اَمْرِیْ فَاصْرِفْهُ عَنِّیْ
وَاصْرِفْنِیْ عَنْهُ وَاقْدِرْلِیَ الْخَيْرَ حَيْثُ كَانَ ثُمَّ اَرْضِنِیْ بِهٖ

**Tafsiri:**
"Ewe Mola, naomba wema katika elimu yako na nina omba uwezo katika kudra yako, na ninakuomba katika fadhili zako kuu, kwani Wewe ndiwe Uwezaye wala mimi siwezi, na Unajua nami sijui, nawe ni Mjuzi wa mambo ya ghaibu. Ewe Mola, kama Unafahamu kuwa jambo hili litakuwa la kheri kwangu katika dini yangu na katika maisha yangu na matokeo yake ni mema, basi nikadirie katika jambo hili na Unirahisishie na kisha Unibarikie kwalo, na kama Unajua kuwa jambo hili litakuwa la shari kwangu katika dini yangu na maisha yangu na matokeo rake si mema, basi litenge mbali nami na Unitenge mbali nalo na Unikadirie jambo la kheri po pote lipatikanapo na Unifanye nitosheke nalo".

Baada ya kusoma dua hii Mtume s.a.w. alisema jambo alilokuwa nalo, na alipomaliza Sala alikwenda kulala.

Seyyidina Ahmad a.s. Masihi Aliyeahidiwa, Mwanzilishi Mtakatifu wa Jumuiya ya Ahmadiyya alihimiza sana jambo hili kwa Wafuasi wake akasema:-
"Mtakuwa wakweli mtakaposhika njia hii, yaani katika kila kitendo na kila taabu kabla ya kushika shauri lolote fungeni mlango wenu kiagukieni kizingiti cha Mwenyezi Mungu na ombeni kwake kwa unyenyekevu: Ee Mola wetu, tumepata taabu hii, kwa fadhili Zako tuondolee. Ndipo roho takatifu itateremka kwenu kuwasaidieni na wakati ule mtafunguliwa njia ya msaada kwa siri" (Safina ya Nuhu, ukurasa 16).
Basi wasomaji wapenzi kwa kushika njia hii waowanao wawili kabla ya kukata shauri lao wanaweza kupata mwongozo. Pengine inawezekana mtu baada ya kuomba akaonyeshwa katika ndoto matokeo ya jambo au pengine inawezekana

anapoamka akasikia utulivu sana moyoni, ambayo ni dalili ya heri. Na inawezekana pia kama jambo si la heri, Mwenyezi Mungu akatia vizuizi vingi hata jambo lisifanyike na livunjike kabisa. Ilimuradi kwa kumwomba Mwenyezi Mungu, mtu analiweka jambo lake mikononi Mwake na Mungu Afanye vile Anavyoona inafaa.

## KUFUNGA NDOA

Mlinzi au Walii wa msichana ni baba yake au baba mdogo au kaka yake au ye yote katika jamaa zake mwanamume anayemwangalia. Na endapo ni mwanamke aliye katika ulinzi wake mwenyewe, Walii atakuwa yule mwenye madaraka katika Serikali kama vile hakimu.
Mlinzi wa msichana baada ya kutaja mahari ya binti yake au nduguye huchaguliwa siku maalum ya kufunga ndoa. Mahali pa kufunga ndoa, awepo mlinzi mwanamume na mashahidi wawili, ijapokuwa si lazima binti awepo. Kwani
binti huulizwa tu na wazazi wake na aishapo kutamka kuwa amekubali ndipo ndoa hufungwa. Na vile vile kwa dharura tu, kama mume haiwezekani awepo anaweza kumchagua mtu fulani wa kumsimamia katika kufunga ndoa. Hapo, kabla ya ndoa kutangazwa ilikuwa desturi ya Mtume wetu Muhammad s.a.w. kusoma hotuba. Hotuba katika ndoa husaidia kuitangaza ndoa na kuifanya kuwa katika hali takatifu zaidi. Na hotuba ya ndoa ni hii ifuatayo kama alivyokuwa akiitoa Mtume s.a.w.

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ نَحْمَدُهُ وَنَسْتَعِيْنُهُ وَنَسْتَغْفِرُهُ وَنُؤْمِنُ بِهٖ وَ
نَتَوَكَّلُ عَلَيْهِ وَنَعُوْذُ بِاللّٰهِ مِنْ شُرُوْرِ اَنْفُسِنَا وَمِنْ سَيِّاٰتِ

أَعْمَالِنَا مَنْ يَّهْدِهِ اللهُ فَلَا مُضِلَّ لَهُ وَمَنْ يُّضْلِلْهُ فَلَا هَادِيَ
لَهُ وَنَشْهَدُ اَنْ لَّا اِلٰهَ اِلَّا اللهُ وَحْدَهُ لَا شَرِيْكَ لَهُ وَ نَشْهَدُ
اَنَّ مُحَمَّدًا عَبْدُهُ وَرَسُوْلُهُ يٰاَيُّهَا النَّاسُ اتَّقُوْا رَبَّكُمُ الَّذِىْ
خَلَقَكُمْ مِّنْ نَّفْسٍ وَّاحِدَةٍ وَّخَلَقَ مِنْهَا زَوْجَهَا وَبَثَّ مِنْهُمَا
رِجَالًا كَثِيْرًا وَّنِسَآءً وَاتَّقُوا اللهَ الَّذِىْ تَسَآءَلُوْنَ بِهٖ وَ
الْاَرْحَامَ اِنَّ اللهَ كَانَ عَلَيْكُمْ رَقِيْبًا ○ يٰاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوا
اتَّقُوا اللهَ وَقُوْلُوْا قَوْلًا سَدِيْدًا يُّصْلِحْ لَكُمْ اَعْمَالَكُمْ وَ
يَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوْبَكُمْ وَمَنْ يُّطِعِ اللهَ وَرَسُوْلَهُ فَقَدْ فَازَ فَوْزًا
عَظِيْمًا ○ يٰاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوا اتَّقُوا اللهَ وَلْتَنْظُرْ نَفْسٌ مَّا
قَدَّمَتْ لِغَدٍ وَاتَّقُوا اللهَ اِنَّ اللهَ خَبِيْرٌ بِمَا تَعْمَلُوْنَ ○

Baada ya kusomwa hotuba hii na mmoja wa waliohudhuria au Kiongozi wa dini, ndoa hutangazwa kuwa fulani bin fulani anamwoa fulani binti fulani kwa mahari kiasi kadha. Na halafu mlinzi huulizwa naye akasimama kusema kuwa “nimekubali kumwoza binti yangu kwa fulani bin fulani kwa mahari kiasi kadha”. Kisha mume naye huulizwa na kusimama kusema “nimekubali kumwoa fulani binti fulani kwa mahari kiasi kadha”. Kisha baada ya hapo ndoa huwa imekwisha fungwa, na watu hula tamutamu kama ilivyokuwa desturi ya Mtume s.a.w.

## WALIMA

Kwa desturi ya Mtume Muhammad s.a.w. mke aendapo kwa mumewe na ikawa wamekwisha kuingiliana mume huandaa karamu na kuwaarifu jamaa na rafiki zake waje kula. Lakini haijuzu kula walima kabla hawajaingiliana. Safari moja Mtume s.a.w. alipoona alama ya rangi ya manjano aliyokuwa nayo Bwana Abdur-Rahman bin Auf, aliuliza na akaambiwa kuwa Abdur-Rahman bin Auf ameoa. Hapo Mtume s.a.w. akamwambia afanye walima (yaani karamu) ijapokuwa kwa mbuzi mmoja. Katika ndoa yake mwenyewe Mtume s.a.w. alikuwa akifanya walima. Safari moja alimwoa Bi Safiyya na aliporudi kutoka Khaibar alifanya walima kawaarifu rafiki zake kila mmoja aje na chakula chake mwenyewe kutoka nyumbani kwake na wote wakakusanyika mahali pamoja wakala chakula kwa ajili ya arusi. (Bukhari).

Hadithi hii inatufunza kuwa kama mtu hana uwezo kabisa wa kufanya walima anaweza, kuwaarifu rafiki zake waje kila mmoja na chakula chake na wale pamoja, kama vile Mtume s.a.w. alivyofanya kwa kuwa alikuwa safarini.

Mume aishapo kumjua mke wake ndipo mahari hutolewa. Kama ilivyoelezwa katika Kuran Takatifu".
"Na kwa ajili ya faida mnayoipata kwao, basi wapeni mahari zao zilizolazimishwa" (Sura 4 Aya 25).
Aya hii inueleza kuwa mahari ni jambo la lazima kwa ajili ya faida anayoipata mume kwa mkewe. Nayo mahari ni haki ya mke.
Desturi zilizo kinyume kabisa na mafundisho ya Kiislam zimeenea katika nchi za Afrika ya Mashariki juu ya jambo hili

la mahari. Mahari inapotolewa basi wazazi wa mke huchukua na kuigawanya bila idhini ya binti yao. Si haki kufanya hivi kwa mujibu wa Islam. Islam inafundisha kuwa mahari ni mali ya mke. Kwa hivi kama binti mwenyewe aseme kuwa kwa mahari yake vitu fulani vinunuliwe, hili ni shauri jingine. Waila kama asiseme, basi hakuna akili ya kunyanganya katika haki yake.

**Kumla ujana mke:**

Jambo la kumla ujana mke ni mojawapo ya matatizo yanayowakabili watu wengi. Mambo mengi ya mila za watu ambayo Dini ya Islam haikuwaamuru watu kufanya, yanashikwa na baadhi ya watu kwa nguvu hata yanaharibu heshima ya hadhi ya Islam, na hili ni moja wapo.

Siku inayosemwa leo bibi arusi na bwana arusi Watakutana, basi huandaliwa watu wa kuja kwa shangwe na hoi hoi. Usiku uingiapo, maarusi wawili huingia chumbani na kulana ujana. Lakini huwa lazima awepo bibi mmoja ambaye ndiye somo wa bibi arusi ili amwangalie bibie asije akaondoka kitandani kwa kuogopa. Pale kitandani huwekwa kitambaa fulani ili damu ya bikira itakapotoka imwagikie kwacho na hapo vigelegele vipigwe na yule somo kama alama ya kuwafahamisha watu kuwa bibie ana bikira. Kitambaa hicho ama “kisarawanda” kama kijulikanavyo hutembezwa kwa ndugu wa bibie kwa shangwe kuu na nyimbo. Baada ya hapo mume humchukua mkewe nyumbani kwake. Kwa hakika mambo haya ni mbali kabisa na mafundiso ya Islam. Ama kumpeleka kwa kasida za Mtume s.a.w. na sherehe za maandamano yenye staha na utulivu si vibaya.

1. Haijuzu kabisa kabisa mtu mwingine ye yote awepo wakati mume na mke wako faraghani. Jambo la kuwapo mtu mwingine kama msimamizi katika chumba cha bibi na bwana arusi ni jambo la kishenzi na lisilojuzu.
2. Kwa desturi mume anatakiwa kabla ya kumwingilia mkewe, kwanza amfanyie tu mambo ya mahaba ya kumfariji kwa maneno ya mapenzi kwa muda kidogo kabla ya kumwingilia na hapo kama mkewe alikuwa bikira hataona taabu yo yote wala karaha; na wakati wa kuingiliana, wanatakiwa kuomba Mungu awalinde na shetani kwa kile atakachowapa. Ili mtoto akizaliwa awe mtoto mwema. Lakini njia ya kuwapo watu wengine na wote wakawa na shauku ya kujua kuwa kimwana ana bikira au hana, na halafu mambo yaanzwe kutangazwa huko na huko ni kinyume na Ustaarabu licha ya kuwa ni kinyume na mafundisho ya Islam.
3. Mume na Mke wamekatazwa kabisa na sheria ya Islam kueleza habari zo zote za siri ya nyumbani kwao. Na huhesabiwa kuwa maluuni (amelaniwa na Mwenyezi Mungu) mtu anayekwenda huko na huko akieneza habari za mke wake au mume wake.
4. Kweli yawezekana mara nyingi mabibi arusi wawe na bikira lakini hutokea vile vile kwa kutegemea maisha anayoishi msichana na mahali anapokaa msichana akawa hana bikira. Mathalan wasichana wanaosoma shule, wao hucheza michezo mingi ya kurukaruka na hii yote baada ya muda mfupi tu hutatua kidogo kidogo nyuzi za msichana.
Na pia wasichana wanaoishi katika nchi zenye joto kali, baada ya kuvunja ungo kwa muda mfupi kabla ya kuolewa nyuzi zao hujitatukia zenyewe.
Basi kwa ufupi tabia ya kuweka somo au mchunga wakati wa faragha ya bibi na bwana inalaumiwa vibaya sana na Dini ya Islam.

## KIWANGO CHA MAHARI

Kurani Tukufu haikutaja kiwango hasa kinachopasa kutolewa kwa ajili ya mahari. Mahari ni neno la Kiarabu "mahr" ambalo maana yake ni "hidaya", "bakhshishi" au "zawadi". Neno hili limetumiwa katika Kuran kwa kueleza hidaya iliyo wajibu kwa mume kumpa mke wake. Kama sheria ya Mwenyezi Mungu ingeweka kiwango cha mahari huenda ingewawia taabu watu wengine kufunga ndoa kwa sababu ya hali mbali mbali walizo nazo watu. Na kwa hivi Mwenyezi Mungu ameliacha jambo hili mikononi mwa watu wenyewe ili watoleane mahari kwa kujitazama hali zao. Na inapokuwa ni lazima kwa watu kuweka kiasi maalum kwa kadiri ya hali zao inaruhusiwa pia. Mathalan Khalifa wa pili wa Seyyidna Ahmad, Hadhrat Mirza Bashir-ud-Din Mahmud Ahmad (Mungu Awe radhi naye) kwa kuwaona Waahmadiyya kadha wanatoa sehemu fulani ndogo sana kuwa mahari kwa wake zao, yaani baadhi yao walipoanza kufikiri kuwa hata rupia thelathini tu zinatosha kuwa mahari, na wengine wanaweka mahari makuhwa sana zaidi ya uwezo wao yanayowashinda wasiweze kulipa. Hapo alipendelea kuwa ni vizuri mume atoe pato lake la miezi sita kumpa mkewe, haidhuru kama atoe kidogo kidogo au atoe yote mara moja akiweza. Mwenyezi Mungu anasema katika Kuran kuwa:-

"Na wapeni wanawake mahari zao kwa hiba. Lakini wakiwapeni chochote kwa radhi ya nafsi zao katika hayo, basi kileni kwa furaha na kunufaika" (Sura 4 Aya 5).

Katika Aya hii Mwenyezi Mungu ametoa mwongozo mzuri sana.

(I) Ametoa mwongozo kwa mume kwamba ni lazima atoe mahari kwa maridhawa na kwa hiba. Endapo mtu mathalan pato lake la kila mwezi ni zaidi ya Sh.800/= haijuzu aseme ati

atatoa mahari Sh.100/= tu. Hapo anaambiwa atoe mahari kwa mke wake kwa hiba. Kwa wakati huo huo wazazi wa mke wanafahamishwa kuwa hawana haki ya kumlazimisha mkwe wao kutoa mahari asiyoweza. Pengine anapata Sh.100 tu kwa mwezi, hivyo haistahiki kumwambia atoe Sh.800/=. kwani jambo hili litamfanya mkwe wao atoe mahari shingo upande au pengine ashindwe kabisa, kwa mujibu wa Islam mkwe wao akishindwa hukumu yake ni kwamba wanampa wao wenyewe shida binti yao.

(2) Ametoa mwongozo kwa mke pia kwamba kwa kutazama jinsi anavyompenda mumewe anaweza pia kummegulia sehemu fulani ya mahari yake. Na mume asione vibaya kuitumia mali apewayo na mke wake.

(3) Kwa kupewa mahari, mke anakuwa na haki na madaraka kwa mumewe kama alivyo mume kwa mkewe.

Mahari inamfahamisha mke kuwa ni lazima sasa ajifahamu kuwa ni mtu mwenye madaraka nyumbani kwake. Hana budi aangalie kila kitu kllichomo mikononi mwake kwa ajili ya mume wake. Na wakati huo huo mume kwa kuloa mahari anafahamishwa kuwa mkewe ni jamaa yake wala si mtumishi wake, na hana budi kumtimizia mapenzi kama inavyostahili na kumfahamu kuwa ni mwenye haki ya kutumia kila kilicho haki yake.

## MKE NA MUME WANA WAJIBU GANI?

Wajibu wa mume kwa mke wake na wa mke kwa mume wake ndiyo mas'ala yetu nyingine yenye maana sana.
Kwani wajibu wa mtu ndicho kitu kinachoweza kumfanya aendelee kukaa na mwenziwe, na mara mtu aachapo kile kinachompasa kufanya, taabu inaingia na mwishowe mfarakano.

(1) Mume hana budi kumfahamu mkewe kuwa ni mpenzi wake na jamaa yake. Na ndoa yao hasa imesimama katika shabaha ya mapenzi. Kama aanze kumtendea mkewe mambo ambayo kwayo mapenzi ya mkewe yatahafika, afahamu kuwa atashindwa kutimiza makusudio ya ndoa.
Mtume s.a.w. alisema:
"Mbora wenu ni yule katika ninyi amtendeaye mema zaidi mke wake (Muslim).
"Kila mmoja wenu ni mchungaji, na kila mmoja wenu ataulizwa juu ya raia zake; mfalme ni mchungaji, na mwanamume ni mchungaji wa watu wa nyumbani kwake, na mwanamke ni mchungaji wa nyumba ya mume wake na watoto wake, basi kila mmoja wenu ni mchungaji na kila mmoja ataulizwa juu ya raia zake" (Bukhari).
"Enyi watu wangu! mna wajibu fulani fulani juu ya wake zenu kama wao walivyo na wajibu juu yenu. Wake zenu ni amana ya Mwenyezi Mungu iliyo mikononi mwenu, kwa hiyo ni lazima mwatendee mambo yote yaliyo mema" (Muslim).
"Na angalieni sana wajibu wenu kwa Mwenyezi Mungu juu ya wanawake, kwani mmewachukua kama amana ya Mwenyezi Mungu, nao wana wajibu kwenu kwamba hawatamruhusu ye yote msiyempenda kuingia katika nyumba zenu, na kama

wakifanya hivyo basi wapeni adhabu ndogo isiyoweza kuacha alama zo zote katika miili yao" (Muslim).

Hadithi hizi zote zinamfundisha mume na mke kuangalia wajibu wao kila mmoja kwa mwenziwe. Na zinatia mkazo sana kwamba mume ni lazima afahamu kuwa mke wake ni amana ya Mwenyezi Mungu aliyoichukua, na kwa hivi atakuja ulizwa na Mwenyezi Mungu juu ya amana hiyo. Watu wengine wana desturi mbaya sana ya kwamba wake zao wanapowakosea, mara tu huanza kuwapiga sana hata ikawa lazima mke aende hospitali. Jambo hili ni kinyume na limelaumiwa sana na mafundisho ya Islam. Mnaweza kupimia wenyewe kuwa mama anazaa mtoto kwa machungu na taabu kubwa sana, lakini hata hivyo hana haki wala uhuru wa kumfanya apendayyo, sembuse mkeo aliye ni amana kwako, uliyemchukuwa kwa masikilizano na mapenzi?

(2) Mke kwa jumla ana wajibu sawa na ulivyoelezwa, katika Hadithi hizo nilizotaja. Yaani hana budi kuangalia kila kitu cha nyumbani kwake na kukiweka katika hali njema. Mke haijuzu kwake atumie mali ya mume wake kwa fujo ingawa anayo haki kuitumia. Na ni juu ya mke kuichunga heshima ya mume wake na heshima yake mwenyewe na kuwa mke mstahiki.

Ama mambo yote yaliyo lazima kwa mwanamume juu ya amri za Mwenyezi Mungu ndiyo yaliyo lazima kwa mwanamke pia. Kwa hiyo ni lazima mke aishi maisha hasa ya kumridhisha mume wake sawa na sheria ya Mwenyezi Mungu. Kwa kujichungia heshima yao wanawake, Mwenyezi Mungu ametoa amri katika Kuran Tukufu:

"Ewe Nabii, waambie wake zako na mabinti zako, na wake wa waaminio wateremshe juu yao shungi zao. Hivyo inaelekea

zaidi wajulikane na wasiudhiwe. Na Mwenyezi Mungu ni Msamehevu, Mrehemevu”. (Sura Aya 60).

“Wateremshe juu yao shungi zao, yaani shungi ziteremshwe hata zifunike nyuso, Katika tafsiri ya Aya hii imesemwa. “Wafunike nyuso zao na miili yao kwa nguo kubwa watakapotoka nje kwa haja”. (Baidhawi). Ibin Abbas anasema. “Mwenyezi Mungu amewaamrisha wanawake Waislam watakapotoka nje kwa haja waangushe nguo kutoka kichwani na kufunika nyuso zao”. (Ibn Jarir).

Maovu mengi ya ufasiki yanayoleta uadui baina ya Watu, na kuwaondolea starehe na utulivu wa moyo, yanatokana na kupuuzwa amri hizi. Amri hizi zimekusudiwa kuing’oa kabisa mizizi ya maovu haya. Watu wataendelea kuwa katika mashaka maadamu hawatii amri hizi za Mwenyezi Mungu. Waislamu wanatakiwa kufanya kila juhudi, wake kwa waume kuona ya kuwa maagizo haya ya Mwenyezi Mungu yanafuatwa kwa uaminifu. Kushikilia mambo ya ada na desturi za watu hakujapata kuleta heri duniani tunapokuta ada hizo zinapingana na hukumu za Mwenyezi Mungu. Mwanadamu hana busara pasipo kuongozwa na Mwenyezi Mungu. Desturi ya kuchanganyika ovyo wanawake na wanaume wasio na mipaka ya kuonana, na kuachwa maagizo yanayoelezwa na Aya hizi. ndiyo mambo yanayoimarisha maovu ya aina hii duniani; nayo ni moto unaounguza nyoyo na kuziteketeza, na kumfikisha mtu katika Moto mbaya zaidi siku ya Kiyama.
Kwa hali yo yote ni lazima mwanamke aangalie ya kuwa heshima ya mume wake imo mikononi mwake. Na kwa kuzilinda heshima hizi, mahali pengine katika Kuran Mwenyezi Mungu Amesema:-

Waambie waaminio wanaume wainamishe macho yao, na wazilinde tupu zao, hili ni takaso kwao; Bila shaka Mwenyezi Mungu Anazo habari za yale wanayoyafanya.

Na waambie wanawake waami-nio kwamba wainamishe macho yao na wazilinde tupu zao, na wasidhihirishe uzuri wa sura zao wala mapambo yao isipokuwa yale yaliyo bayana katika hayo, na kwamba washushe shungi zao mpaka vifuani mwao, na wasionyeshe uzuri wa sura zao wala mapambo yao isipokuwa kwa waume zao, au kwa baba zao au kwa baba za waume zao, au kaka

zao au wana wa kaka zao au wana wa dada zao au wanawake wenzao au wale waliomilikiwa na mikono yao ya kuume au wale miongoni mwa watumishi wa nyumbani wa kiume ambao hawana uovu nafsini mwao, au watoto wadogo ambao hawajafikia umri wa kuwa na wazo lo lote kuhusu sehemu za siri za wanawake. Na wasitembee kwa namna ambayo inafichua uzuri waliouficha. Na tubieni nyote kwa Mwenyezi Mungu enyi waaminio, ili mpate kufaulu. (Sura 24 Aya 31 na 32)

Aya hizi zilizoandikwa hapo juu zinaeleza mafundisho yanayoweza kumpa mtu usafi wa moyo. “Mapambo”. Neno hili Kiarabu ni “ziinat” ambalo lina maana ya mapambo, na kila sehemu inayoshawishi na kuvutia ya mwanamke, kama umbo lake na uso na uzuri wa mwili n.k.w.

“Isipokuwa yale yaliyodhihirika”, yaani yaliyolazimika, yasiyo katika uwezo wa mwanamke, kama mathalan hana nguo, au kwa sababu ya ugonjwa, au kwa sababu ya kazi na mengineyo.

“Waangushe shungi zao” yaani shungi zitoke kisogoni zipite juu ya kichwa, zifunike uso, zishuke mpaka vifuani. Lakini wanaweza kuonyesha mapamho yao kwa jamaa zao ambao ni hao tu waliotajwa katika Aya hii. “Wanawake wao”.

Wanawake wengine wasio jamaa zao wamekatazwa kuchanganyika nao. Maana wanawake mara nyingi wamekuwa sababu ya fitina. Hufika majumbani na kupeleka nje habari za wanawake wanaowaona. Aya hii imewakatalia wanawake pia kuingia ovyo majumbani mwa watu, na kadhalika wanawake waaminio wamekatazwa kuonyesha mapambo ya uzuri wao kwa wanawake ovyo.

"Wala wasipige miguu yao". Inaonyesha kuwa ngoma na dansi na michezo ya namna hii imekatazwa.

Kwa ufupi haya ni mambo muhimu ambayo mume na mke wake yawapasa kuzingatia sana na kuangalia kuwa wanayatimiza ili kwanza wapate radhi ya Mwenyezi Mungu na kwa wakati huo huo wazidishe furaha yao na
waweze kutimiza hasa makusudio ya ndoa yao.

## WANAWAKE WALIO HARAMU KUWAOA

Sheria ya Mwenyezi Mungu imekusudiwa kumfanya mwanadamu aweze kuonekana hasa kuwa ni kiumbe bora kabisa tofauti na wanyama. Pasipo sheria zozote za Mwenyezi Mungu kuletwa duniani binadamu wangeishi kama wanyama tu na ingekuwa hakuna tofauti kubwa baina ya mnyama na mwanadamu. Basi katika jambo la kuingiliana mwanamume na mwanamke. Mwenyezi Mungu Hakuwaacha wanadamu wajifanyie vile wanavyotamani tu kama wanyama, bali ameweka taratibu maalum ya fungamano la ndoa baina ya mwanamke na mwanamume.

Na vile vile basi amemwekea mwanadamu mipaka ya kufanya fungamano hilo ili heshima ya binadamu ipatikane. Katika sheria ya Dini ya Islam, mwanamume haruhusiwi kufunga ndoa na

wanawake hawa wafuatao kama alivyokataza Mwenyezi Mungu katika Kuran:-

Mmeharimishiwa (kuoa) mama zenu, na binti zenu, na dada zenu, na shangazi zenu, na dada za mama zenu, na binti za ndugu, na binti za dada, na mama zenu waliowanyonyesheni, na dada zenu wa kunyonya, na mama za wake zenu, na binti zenu wa kambo walio katika ulinzi wenu, waliozaliwa na wake zenu mliowaingilia - lakini kama ninyi hamjawaingilia, basi si vibaya kwenu (kuwaoa) - na wake wa wana wenu waliotoka katika migongo yenu; na (imeharimishwa) ya kwamba mwaoe madada wawili wakati mmoja, isipokuwa yale yaliyokwisha pita; hakika Mwenyezi Mungu ndiye Msamehevu, Mrehemevu. Na pia (mmeharimishiwa) wanawake wenye kuolewa, isipokuwa wale iliyowamiliki mikono yenu ya kuume. Ndiyo sheria ya Mwenyezi Mungu juu yenu. Na mmehalalishiwa (kuoa wanawake) minghairi ya hao, kwamba mwatafute kwa mali zenu, kwa kuwaoa bila ya kufanya zinaa, Na kwa ajili ya faida mnayoipata kwao, basi wapeni mahari zao zilizolazimishwa; wala si vibaya kwenu katika yale mli yoridhiana baada ya (kutoa) mahari. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi, Mwenye hekima. (Sura 4 Aya 24 na 25).

Kuran inapoeleza upande mmoja inakuwa kwa wakati huo huo inaeleza upande wa pili; Wanaume wameharimishiwa kuoa wanawake waliotajwa katika Aya hizo mbili, lakini ni juu ya wanawake pia kuangalia kuwa wao ikiwa wanao uhusiano na wanaume sawa na hao waliotajwa katika aya hizo, wasikubali kuolewa wala wasitake kuolewa nao. Huenda mwanamume hajijui ana uhusiano gani na mwanamke na kwa kumpenda amemtaka kumwoa, basi hapo kama mwanamke atafahamu

uhusiano huo sawa na uliotajwa katika Kuran na akakubali kuolewa ni yeye atakayekuwa na makosa.

Mfahamu pia katika Dini ya Islam si mwanamume tu anayeruhusiwa kumtaka mwanamke kumwoa, bali mwanamke pia anaweza kumtaka mwanamume kumwoa (Bukhari 67:33). Na pia wazazi wa mwanamke wanaweza kumtaka mvulana fulani amwoe binti yao. Hivyo kwa mipaka hiyo ya Mwenyezi Mungu katika kulinda heshima yao, wote wanatakiwa kuangalia, tangu mwenye kutaka mpaka mwenye kutakiwa.

## HARAMU KUFUNGA NDOA NA WASHIRIKINA

Waaminio wamekatazwa kufunga ndoa na washirikina, Kuran inasema:-
"Wala msiwaoe wanawake washirikina mpaka waamini. Na bila shaka mjakazi mwenye kuamini ni bora kuliko mwanamke mshirikina ingawa awapendezeni. Wala msiwaoze wanaume washirikina mpaka waamini", (Sura 3 Aya 222).
Waislamu wamekatazwa kuwaoa wanawake washirikina na kuwaoza washirikina binti zao, maana kwa kufanya hivyo inaweza kuleta hatari juu yao na juu ya watoto wao, na wanaweza kupotea bure. Mwenyezi Mungu amekwisha kuwaokoa katika uchafu wa ushirikina, kwa nini kujiingiza tena katika taabu zile za zamani.

## KUOA ZAIDI YA MKE MMOJA

Kiwango cha wake katika Dini ya Islam kimefanywa kuwa wake wanne. Kwa kutazama hali mbalimbali Mwenyezi Mungu Aliyemwumba mwanadamu na umbile lake lote, Ameruhusu kwamba endapo mtu ana haja fulani fulani za halali na kwa kuishi na mke mmoja tu itamwia taabu, basi anaweza kuoa zaidi ya mke mmoja mpaka wawili na watatu na mwisho kabisa wanne. Imesemwa katika Kuran kuwa:-
"Basi oeni mnaowapenda katika wanawake, wawili na watatu na wanne. Lakini mkiogopa kuwa hamwezi kufanya uadilifu basi (oeni) mmoja tu", (Sura 4 Aya 4).

**Sababu za kuoa wake wengi:**

Sababu za ndoa zilizoelezwa na Kuran ni nne:
(1) Kujilinda na maradhi ya kimwili na ya kiroho na kuweka murua mwema, kwa kumfanya mtu awe na uwezo wa kutosha kujiepusha na zinaa. (Sura 4 Aya 25).
(2) Kupata utulivu wa moyo na kuwepo mwenzi mwenye mahaba, na kuwepo stara na starehe kama zinavyostiri libasi. (Sura 30 Aya 22 na Sura 2 Aya 88).
(3) Kuzaa watoto na kukuza taifa la watu. (Sura 2 Aya 224).
(4) Kupanua ujamaa na nasabu. (Sura25 Aya 55).
Hivyo basi:-
(a) Kuna wanaume wenye matamanio makali na nguvu kubwa, wao wasingetoshwa na mke mmoja. Islam ingezuia kuoa wake zaidi, watu wenye jinsi hii wasingefaidishwa na dini, na japo wawe na nia ya kujitakasa namna gani, lakini budi wangeshindwa na tamaa hii ambayo ina nguvu kuliko tamaa nyingine.

(b) Kama mke ni mgonjwa-mgonjwa daima, au amelemaa kabisa, au amepata wazimu, au ukoma, mume hawezi kupata utulivu. Kumfukuza mkewe si jambo la
murua na ni aibu kwa vile wamekaa dahari nyingi kwa wema, na sasa ni wajibu wa mume kumwuguza mkewe. Na Dini ya Kiislamu ingekataza kuoa zaidi basi mume huyo angekuwa amedhulumiwa bure na mwishowe angetenda maovu kwa kushurutishwa.
(c) Kama mke ni tasa, na mtu ana haja ya watoto wa kuendeleza jina lake na ukoo wake, bila kuoa mwingine hawezi kamwe kupata starehe ya kufurahi navitoto vya damu yake, na ambavyo pengine vingemfaa vitakapokua, naye kawa mzee na aliyechoka. Hivyo Uislam haukufanya ujinga hata kidogo katika kuruhusu mtu mwenye wasaa wake ajiolee wake mpaka wanne.
Kwa desturi baada ya vita, watu hupungua sana. Leo hii Ulaya haitaweza kupona katika kupungukiwa na wanaume ambao wangehitajiwa katika kupunguza uharibifu uliowaingilia; sharti waachilie mbali maoni yao yenye makosa juu ya jambo hili, wawaruhusu watu kuoa zaidi ya mke mmoja.

Siku hizi Wakristo wenye maarifa wamekwisha kubali kabisa kuwa kuoa wake wengi ni lazima kwa mwanadamu. Kwa mfano mtaalamu mmoja Mzungu Bwana Sapiens aliandika makala moja katika gazeti la “East African Times” la mwezi September 1959 kuwa, *“Polygamy is a natural and, to my mind, most necessary system of living. Monogamy is the child of poverty”*, yaani “Kuoa wake wengi, nionavyo mimi, ni jambo la kiasili na ni taratibu ya lazima kabisa ya maisha. Desturi ya kuoa mke mmoja imezalikana na umaskini “. Mtaalamu huyo akaendelea, kutoa sababu kubwa zinazoonyesha ni lazima

mtu aruhusiwe kuoa wake wengi. Akaandika:-
I. Wanaume na Wanawake waliumbwa na Mwenyezi Mungu ili wawe wenye kujistahi, wafanye kazi kwa kusaidiana na kukaa pamoja kama mke na mume.
2. Kuna wakati ambapo mwanamke anakuwa hawezi kutimiza wajibu wake wala hawezi kufanya shirika na mume, mama-watoto wasioolewa walla magonjwa mabaya.
3. Katika kuoa mke mmoja tu hapo inamwia taabu sana mume hata anayaona maisha kuwa magumu sana.
4. Katika wakati wote huo hata awe mume mwenye tabia ya namna gani ataanza kutafuta na kupata njia ya kujisaidia kutimiza tamaa ya mwili, na hapo ndoa ya mkewe huvunjika mara moja: na hasara itakayopatikana baada ya kufanya hivi ni kwamba watapatikana watoto wa haramu, mama-watoto wasioolewa na magonjwa mabaya.

Hizi ni baadhi ya sababu zake saba alizozitoa. Nasikitika sina nafasi ya kuziandika zote. Nitaomba radhi sana, kuwasihi sana wale jamaa wapenzi wenye dini zinazokataza kuoa wake wengi ati kwa maana ya kuwa wake wengi ni chukizo mbele ya Mungu, wasihuzunike bali wafurahi na kushangilia kuwa shauri ninalowapa la kuitakia wema nchi haliendi kinyume na makusudio hasa ya dini zao. Dini hizo kwa kutoa mafundisho haya ziliwatakia watu yaliyo mazuri, hazikuwatakia mabaya, basi hatuwezi kuzilaumu kwani nia yao ilikuwa nzuri, maana zilidhani va kwamba kwa njia hii watu wataona raha zaidi kama waoane na wakae na mke mmoja mmoja. Lakini sasa kukaa na mke mmoja bila sababu hasa si raha bali hatari kubwa kwa ajili ya taifa zima, hivyo shauri langu halikupingana na nia hasa ya dini hizo ya kuwatakia watu yaliyo mema. Juu ya hayo watafurahia kusikia ya kwamba katika Afrika ya Magharibi

Wakristo wamepewa ruhusa kuoa zaidi ya mke mmoja, basi huku pia tunahitaji sana ruhusa kama hiyo kwa wakuu wa dini hizo ili tuitengeneze hali yetu.

## TALAKA

Neno talaka ni neno “talaaq” la Kiarabu ambalo lina maana ya kuacha au kufungua fundo. Na wanazuoni wanalifasiri neo hili kwa maana ya “khul`a” yaani kukiondoa kitu kutoka mahali au kukichukua kutoka mahali fulani. Neno hili katika dini ya Islam limetumiwa kwa maana ya kuachana kwa mume na mke. Na juu ya jambo hili Mwenyezi Mungu ametoa katika Qur`an Sura nzima - Suratul —Talaaq.

Kabla ya kuingia katika kueleza jinsi kuachana huku kwa mume na mke kunavyofanywa, tungependa kueleza machache juu ya kuachana kwenyewe. Machoni pa watu wengine mume na mke kuachana ni jambo lisilokubaliwa. Lakini katika Dini ya Islam hakuna sheria yoyote ya Mwenyezi Mungu inayomlazimisha mtu kufanya vile asivyoweza kufanya. Anasema Mwenyezi Mungu katika Qur‘an:- “Mwenyezi Mungu Haikalifishi nafsi yoyote ila yaliyo sawa na wasaa wake; (faida ya) yale iliyoyachuma ni yake na (hasara ya ) yale iliyoyachuma ni juu yake.” ( Sura 2 aya ya 287).

Watu wengine hufikiri vibaya sana kwamba Dini ya Islam kwa kuruhusu kuachana basi ndiyo kusema inapendelea kuachana. Masikini wanashindwa kupambanua baina ya kuruhusu na kupendelea. Hakika ni hii tu ya kwamba Dini ya Islam inapendelea watu wasiachane kabisa baada ya kuoana, kwani hayo hasa ndiyo makusudio ya ndoa. Lakini imetoa nafasi kuachana endapo mke na mume hawawezi kabisa kusikilizana na wala hakuna tena mapenzi, na hata kila mmoja

anaona kama vile nyumba yao imegeuka kuwa moto. Hapo Islam haiwang'ang'anizi kukaa pamoja, bali inatoa ruhusa waachane ili kila mmoja apate furaha. Basi kufikiri kuwa maadamu Islam inaruhusu kuachana ndiyo basi tusema inapendelea ni kosa kubwa, maana Mtume wetu Muhammad s.a.w. alisema wazi wazi:- "Mwenyezi Mungu hakuchukia kitu kingine zaidi katika vitu alivyo halalisha kama kuachana kwa mume na mke wake." (Abu Daud 13:3).

Hadithi hii inatufundisha kuwa kuachana kumeruhusiwa tu kwa vile hali za wanadamu siku zote hubadilika - badilika, hivyo kwa kukataa kutupa taabu zaidi kwa kajambo ka upuuzi tu hivi mara hivi mara mume na mke wakasirikiane na kutaka kuachana. Bali ni kwa mambo ambayo kwa vyovyote wanashindwa kabisa kabisa kupatana.

## KUPATANISHWA WAGOMBANAO

Iwapo mume na mke hawapatani juu ya jambo watawaita watu wawili; mmoja wa upande wa mke na mwingine wa upande wa mume ili baada ya kuchungua ugomvi wao wajaribu kila njia kuwapatanisha na endapo hawakupatana basi wenyewe sasa wataamua kama kuachana au kupatana na kukaa pamoja kama desturi. Qur'an Tukufu inaeleza kuwa:- " Na kama mkihofia ugomvi ulio baina yao, basi wekeni hakimu mmoja katika jamaa za mwanamke. Kama wote wawili wakitaka mapatano. Mwenyezi Mungu Atalinganisha baina yao; hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi, Mwenye habari." (Sura 4 aya 36).

"Na kama wakitengana, Mwenyezi Mungu atawastawisha kila mmoja wao kwa wasaa wake. Na

Mwenyezi Mungu ni Mwenye wasaa, Mwenye hekima." (Sura 2 aya 131).

Aya hizi zinatufundisha ya kuwa: inapokuwa Mke na mume wameshindwa kabisa kabisa kuendeleza maisha yao pamoja, basi jambo lililo zuri kwao ni kwamba watengane; na Mwenyezi Mungu ameahidi kumnufaisha kila mmoja kwa kumpatia mwenzi wa kumfaa.

## JINSI YA KUACHANA

Mwenyezi Mungu ameeleza katika Qur 'an kuwa:- Kwa wale wanaoapa kwamba watajitenga na wake zao (muda wao) ni kungoja miezi minne; na kama wakirejea, basi hakika Mwenyezi Mungu ni Msamehevu Mrehemevu." (Sura ya 2 aya 227).

Aya hii inaeleza kuwa mtu anapoapa kuwa hatakaribiana na mkewe; katika hali hii mume hawezi kumwacha mkewe kwa muda wa zaidi ya miezi minne. Kama hakuchukuwa mke wake katika muda huo, basi ikipita miezi minne itakuwa ni talaka.

Desturi hii ilienea zamani katika Bara Arabu ya kwamba mume aliweza kuapa kwa mkewe kwamba hataingiliana naye, basi Mwenyezi Mungu kwa ajili ya watu hawa wenye desturi ya namna hii ametoa muda ni miezi minne tu, ikipita basi huwa talaka.

"Na wanawake waliopewa talaka wangoje mpaka hedhi tatu, wala haiwapasi kuficha Aliyoumba Mwenyezi Mungu katika matumbo yao, ikiwa wanamwamini Mwenyezi Mungu na siku ya Mwisho; na waume wao wana haki zaidi ya kuwarejesha katika muda huo, kama wakitaka isilahi." (Sura 2 aya 229).

Aya hii inaeleza kuwa mwanamke aishapo kupewa

talaka, basi mpaka siku ya hedhi yake zifikapo na kuisha, huhesabiwa talaka moja, hata hedhi ya pili kuwa ni talaka ya pili; mpaka hedhi ya tatu kama mume akimrudia kabla ya kwisha muda wake huwa ni mkewe, lakini hedhi ya tatu ikisha na mume hakumrudia mkewe huwa si mkewe tena, na hapo ndiyo huhesabiwa amekwisha mwacha. Na kama mke ana mimba pia hapa anaambiwa na Mwenyezi Mungu ni lazima aseme ikiwa ni mwaminio. Lakini je, muda wote huu wa kungoja mke atakaa wapi? Qur'an Tukufu inatoa jawabu:-

"Ewe Nabii mnapotoa talaka kwa wanawake, basi toweni talaka katiak wakati wa eda zao, na fanyeni hesabu ya (siku za ) eda, na Mcheni Mwenyezi Mungu, Mola wenu, Msiwatoe katika nyumba zao wala wasitoke wenyewe, mpaka wafanye jambo la ufasiki ulio wazi. Na hiyo ndiyo mipaka ya Mwenyezi Mungu; na anayeruka mipaka ya Mwenyezi Mungu, basi hakika amejidhulumu nafsi yake. Hujui ya kwamba labda Mwenyezi Mungu Atatokeza jambo jingine baada ya haya."

Basi wanapofikia muda wao, ndipo wawekeni kwa wema, au farakaneni nao kwa wema, na mshuhudishe mashahidi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Hivyo ndivyo anaagizwa yule anayemwamini Mwenyezi Mungu na siku ya Mwisho; na anayemwogopa Mwenyezi Mungu (Mwenyezi Mungu) humtengenezea njia ya kuokoka." (Sura 65 aya 230.

Aya hii inaonesha kuwa mwanamke anaweza kujikomboa kwa kudai talaka mikononi mwa Hakimu, kwa sharti ya kwamba atoe mahari ile aliyopewa na mumewe endapo Hakimu akiona ni sawa. Na kile atakachotoa kwa kujikomboa mwanamume anaambiwa si vibaya kukipokea. Kadhalika hapo inaonesha kuwa mwanamume anaweza pia kumsamehe mtalaka wake kwa kutazama hali yake, yeye halazimishwi kuchukuwa, bali mwanamke ndiye aliyelazimishwa kutoa mahari aliyopewa . Basi kama mume

aone kuwa haili ya mtalaka wake si nzuri huko kwao, pengine hana baba wala mama, wala hana chochote anachotegemea kumwendeshea maisha yake katika hali hii mume aliye ni mcha Mungu hasa anatakiwa kumsamehe ijapokuwa ni haki yake.

Mtu akimwacha mkewe mahari hairudishwi. Qur'an inasema: "Wala si halali kwenu kuchukuwa chochote mlichowapa wake zenu." (Sura 2 aya 230). Aya hii inaeleza kuacha kwa mwanamke na mume wake kwa njia ambayo mume mwenyewe ndiye aliyetaka kumwacha mkewe. Katika kuacha hivi mume hatakiwi kudai mahari yake., bali hasa inatakiwa kumsaidia mkewe kwa hali iliyo sawa na hali yake kama asemavyo Mwenyezi Mungu katika Qur'an Tukufu.

"Si dhambi kwenu kama mkiwapa wanawake talaka ambapo hamjawagusa au kuwawekea mahari. Na wapatieni matumizi - mwenye wasaa kadiri awezavyo na mwenye dhiki kadri awezavyo - matumizi kwa sheria; ndiyo wajibu wa wafanyao wema."

Na kama mkiwapa talaka kabla ya kuwagusa, na mmekwisha wawekea mahari basi (wapeni) nusu ya mliyoyaweka." (Sura 2 aya 237).

Aya hizi zinaonesha kuwa mume amwachapo mkewe hana budi kumpa fedha kidogo au chochote kile cha kumzawadia kadri ya uwezo wake. Na endapo amemwacha wakati hajamwingilia atampa mkewe nusu ya mahari aliyoahidi kutoa wakati wa kufunga ndoa."

## MAMBO MENGINE YA MWONGOZO

### Eda ya Kufiwa:

Mwenyezi Mungu anaamuru katika Qur'an Tukufu: "Na wale wanaofishwa miongoni mwenu na kuacha nyuma yao wake, hawa wangoje miezi minne na siku kumi." ( Sura 2 aya 235).

### Haijuzu kuwaita wake zetu "mama"

Qur'an Tukufu inaonya:- " Mwenyezi Mungu hakumwekea mwanadamu mioyo miwili kifuani mwake, wala Hakuwafanya wake zenu mliyolinganisha migongo yao na migongo ya mama zenu kuwa mama zenu, wala hakuwafanya wana wenu wa kupanga kuwa wana wenu hasa, hayo ni maneno yenu ya viivywa vyenu; na Mwenyezi Mungu Husema kweli, naye Huongoza njia." (Sura 33: 5).

Aya hii inakanusha kabisa desturi ya wale wanaowaita wake zao mama. Safari moja Auis bin Saamit kwa kufuata desturi za tangu zamani za Waarabu kabla ya Islam, alimtamkia mkewe Bibi Khaula maneno "Anti alayya kadhahri ummy," yaani "Wewe kwangu ni kama mgongo wa mama yangu." Mke atamkiwapo hivyo huwa haingiliani na mumewe wala huwa hana uhuru wa kutoka katika nyumba ya mumewe, bali huwachwa hivyo hivyo tu bila ya kupata haki ujumba kwa mumewe, iliyokuwa Destiri ya Waarabu. Basi Bibi Khaula alipoambiwa hivyo na mumewe upesi akaenda kwa Mtume s.a.w. na kumpa kisa hiki. Mtume s.a.w. akasema hawezi kuliingilia shauri hili, maana wakati ule hakujashuka amri yoyote juu ya desturi hii. Bibi Khaula akarudi nyumbani kwake na kumshitakia Mwenyezi Mungu. Kwa fadhila zake Mwenyezi Mungu baada ya muda kidogo, Mtume s.a.w. akateremshiwa

Aya hiyo. Na toka wakati ule amri ikaja kutoka kwa Mwenyezi Mungu kuwa atakayemwambia mkewe maneno hayo; basi kama alikuwa na mtumwa ampe uhuru, na kama hana mtumwa afunge saumu miezi miwili mfululizo, waila awalishe masikini sitini, kama asemavyo Mwenyezi Mungu katika Qur`an Tukufu:- "Na wale wanaowaita wake zao mama, kisha wakarudia katika yale waliyoyasema, basi wampe uhuru mtumwa kabla ya kugusana; hayo ndiyo mnaagizwa kwayo; na Mwenyezi Mungu Anajua mnayotenda."

" Na asiyepata (mtumwa) basi afunge saumu miezi miwili inayoandamana kabla ya kugusana, na asiyeweza, basi awalishe masikini sitini; (mmeambiwa) hayo ili mumwamini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake; na hiyo ni mipaka ya Mwenyezi Mungu; na kwa makafiri iko adhabu iumizayo." (Sura 58 Aya 4-5).

**Vibaya Kusingizia uzinifu:**

Desturi ya kuwasingizia wake kwa uzinzi bila ya ushahidi maalum imelaumiwa na Mwenyezi Mungu katika Qur'an Tukufu. Na Qur'an imeweka mipaka kuwa:- "Na wale wanaowasingizia wake zao, na hawana mashahidi ila nafsi zao, basi ushahidi wa mmoja wao utakuwa kushahidilia mara nne kwa kiapo cha Mwenyezi Mungu; ya kwamba bila shaka yeye ni mmoja wa wakweli. Na mara ya tano (aape) kwamba laana ya Mwenyezi Mungu iwe juu yake ikiwa yu miongoni mwa waongo. Na (mkewe) itamwondolea adhabu kwa kutoa ushuhuda mara nne kwa kiapo cha Mwenyezi Mungu ya kwamba huyu (mume) ni miongoni mwa waongo. Na mara ya tano (aape) kwamba hasira ya Mwenyezi Mungu iwe juu yake kama (mumewe) ni miongoni mwa wakwelli." (Sura 24 Aya 7-10).

**Mwenye hedhi asiingiliwe:**

Qur'an Tukufu inaonya :- " Na wanakuuliza juu ya hedhi, Sema: Hiyo ni udhia jitengeni na wanawake katika hedhi, wala msiwaingilie mpaka wametakasika. Na wamapotakasika basi wafikieni katika pale Alipowamuruni Mwenyezi Mungu; hakika Mwenyezi Mungu Huwapenda wanaotubu na wanajitakasa." (Sura 2 Aya 223).

Mtu hana ruhusa kuingiliana na mkewe katika hali ya hedhi, maana jambo hilo linaweza kuwadhuru wote wawili. Baada ya kukatika damu, mtu amekuwa na ruhusa ya kuingiliana na mke wake. Lakni ni bora angoje mpaka ameoga.

## MAAGIZO MEMA KWA WANAWAKE:

Wasomaji wapenzi tusingependa kufunga makala hii kabla ya kuwatoleeni maagizo yenye maana sana ambayo Mjumbe wa Mwenyezi Mungu wa siku hizi za Mwisho, Seyyidna wa Maulana Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. Mwanzilishi Mtakatifu wa Jamia ya Ahmadiyya, aliandika katika kitabu chake " SAFINA YA NUHU" juu ya wanawake ili akina mama wapate maisha yenye fanaka na ustawi katika majumba yao na waume zao. Na maagizo hayo ya maana ni haya yafuatayo:-

"Katika zama zetu wanawake pia wanaingia na kushughulika katika mambo yaliyo kinyuma cha sheria. Wanafahamu kuwa ni vibaya waume zao kuoa wake wengi kana kwamba hawayaamini mafundisho ya Qur`an. Hawajui ya kuwa katika sheria ya Mwenyezi Mungu imo dawa ya kila namna. Lau kama haikuwa katika sheria ya Uislamu ruhusa

na idhini ya kuoa wake wengi isingekuwa dawa ya mahitaji yenye kumletea mtu fikra ya kuoa mke wa pili. Mathalan mke akipata wazimu au akipata ukoma, au akipata ugonjwa wenye kumfanya kuchakaa, au hali nyingine inayompata mwanamke hata awe mwenye kustahili kuhurumiwa. Na pia mwanamume naye awe astahiliye kurehemewa kwa vile hawezi kustahimili kukaa pasipo mke; katika hali hii itakuwa dhuluma juu ya mwanamume kama hakupewa nafasi ya kuoa mke mwingine. Kwa hakika sheria ya Mungu ilipoona hali ya namna hii ikawafungulia wanaume njia. Yaani mwanamume anapokuwa hafai ni haki kwa wanawake kuomba khulaa ( talaka) kwa mkono wa hakimu. Na kuomba khulaa kwa mkono wa hakimu ni sawasawa na talaka.

Sheria ya Mungu imefanana na duka la mwuza dawa. Kama katika duka la dawa haipatikani dawa ya kila ugonjwa duka haliwezi kuendelea vizuri. Basi fikirinia je, si haki kuwa baadhi ya taabu hiyo wanakuwa na haja ya kuoa mke mwingine? Tena faida gani ya sheria isiyokuwa na dawa ya kuondoa kila ugonjwa na kila taabu?

Tazameni katika Injili imeandikwa ya kuwa kutoa talaka ni kwa sababu ya zinaa tu (Mathayo 5:32). wala hazikutajwa sababu nyingi ziletazo ugomvi na udhia baina ya mke na mume. Kwa hivi Wakristo hawakuvumilia upungufu wa sheria yao na kwahiyo katika nchi ya Amerika wakaongeza sheria nyingine wenyewe katika jambo la talaka. Basi sasa kwa sheria hii Injili imetanguka kwa kutenguliwa na Wakristo wenyewe.

Enyi wanawake msihuzunike: kwani kitabu kilichotolewa kwenu hakihitaji kubadilishwa na watu. Maana kama haki za wanaume zilihifadhiwa kitabuni vile vile haki zenu zimehifadhiwa katika kitabu kile kile. Na kama mwanamke haridhii mume wake aoe mke wa pili, basi

anaweza kuomba khulaa (talaka) kwa mkono wa hakimu. Ilikuwa wajibu kwa Mwenyezi Mungu kutaja katika sheria yake hali zote zinazoweza kuwafikia Waislamu, ili isiwe sheria isiyokamilika bali iwe sheria kamilifu. Enyi wanawake msimshitaki Mungu endapo waume zenu wamefunga nia ya kuoa mke wa pili. Bali ombeni ili Mungu awahifadhini katika msiba na balaa hili. Kweli ni mdhalimu mkubwa mume yule anayeoa wake wawili naye hafanyi adili baina yao. Lakini ninyi msiwe wenye kukasirikiwa na Mungu, kwa sababu ya kumwasi kwenu. Kila mtu ataulizwa vitendo vyake. Kama ninyi mtakuwa wema mbele ya Mungu, mume wenu atafanywa mwema.

Ingawa sheria imeruhusu kuoa wake wengi kwa sababu ya mahitaji mbalimbalil, lakini juu ya hayo, mmefunguliwa kanuni ya kadri ya Mungu. Na kama ninyi hamwezi kubeba kanuni ya sheria, basi jipatieni faida kwa dua katika kanuni ya kadri ya Mungu. Sababu kanuni ya kadri inashinda kanuni ya sheria. Jiihadharini na taweni! msipende sana dunia na mapambo yake wala msijisifu kwa sababu ya kabila zenu. Wala msimfanyie dharau mwanamke yeyote. Wala msiombe kwa waume zenu maombi wasiyoweza kuyapata. Jitahidini mwingie kaburini na hali mmetakasika na mmetukuka. Msifanye uvivu katika kutekeleza faradhi za Mungu kama sala na Zaka na nyinginezo. Na tiini waume wenu kwa mapenzi ya roho zenu. Sehemu kubwa ya heshima yao imo mikononi mwenu, basi tekelezeni kazi yenu hii kwa njia nzuri ili mhesabiwe na Mungu katika wanawake wema wanyenyekevu. Msitumie mali kwa fujo wala msitoe mali za waume wenu ovyo, wala msifanye hiyana, wala msiibe wala msisengenye, wala msimsingizie yoyote." ***(Safina ya Nuhu uk. 51-52).***

بِسْمِ اللهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ

## 2. SURA AL-BAQARA

88. Na bila shaka Tulimpa Musa Kitabu na Tukawafuatisha Mitume (wengine) baada yake. Na Tukampa Isa mwana wa Mariamu Ishara zilizo wazi na Tukamsaidia kwa maneno matakatifu. Basi je! kila mara alipowafikieni Mtume kwa yale zisiyoyapenda nafsi zenu, mlijivuna, kundi moja mkalikadhibisha na jingine mnaliua?

وَلَقَدْ آتَيْنَا مُوسَى الْكِتٰبَ وَقَفَّيْنَا مِنْ بَعْدِهٖ بِالرُّسُلِ
وَآتَيْنَا عِيسَى ابْنَ مَرْيَمَ الْبَيِّنٰتِ وَأَيَّدْنٰهُ بِرُوحِ الْقُدُسِ
أَفَكُلَّمَا جَآءَكُمْ رَسُولٌ بِمَا لَا تَهْوٰٓى أَنْفُسُكُمُ اسْتَكْبَرْتُمْ
فَفَرِيقًا كَذَّبْتُمْ وَفَرِيقًا تَقْتُلُونَ ﴿٨٧﴾

222. Wala msiwaoe wanawake washirikina mpaka waamini. Na bila shaka mjakazi mwenye kuamini ni bora kuliko mwanamke mshirikina ingawa awapendezeni. Wala msiwaoze wanaume washirikina mpaka waamini. Na kwa yakini mtumwa mwenye kuamini ni bora kuliko mwanamume mshirikina ingawa awapendezeni; hao wanaita kwenye Moto, na Mwenyezi Mungu Huita kwenye Pepo na samahani kwa amri Yake. Naye Hueleza Aya Zake kwa watu ili wapate kukumbuka.

وَلَا تَنْكِحُوا الْمُشْرِكٰتِ حَتّٰى يُؤْمِنَّ ۚ وَلَأَمَةٌ مُؤْمِنَةٌ
خَيْرٌ مِنْ مُشْرِكَةٍ وَلَوْ أَعْجَبَتْكُمْ ۚ وَلَا تُنْكِحُوا الْمُشْرِكِينَ
حَتّٰى يُؤْمِنُوا ۚ وَلَعَبْدٌ مُؤْمِنٌ خَيْرٌ مِنْ مُشْرِكٍ وَلَوْ
أَعْجَبَكُمْ ۗ أُولٰٓئِكَ يَدْعُونَ إِلَى النَّارِ ۖ وَاللهُ يَدْعُوٓا
إِلَى الْجَنَّةِ وَالْمَغْفِرَةِ بِإِذْنِهٖ ۚ وَيُبَيِّنُ آيٰتِهٖ لِلنَّاسِ
لَعَلَّهُمْ يَتَذَكَّرُونَ ﴿٢٢١﴾

223. Na wanakuuliza juu ya hedhi. Sema: Hiyo ni udhia; basi jitengeni na wanawake katika hedhi, wala msiwai-ngilie mpaka wametakasika. Na watakapotakasika, basi wafikieni katika

وَيَسْئَلُونَكَ عَنِ الْمَحِيضِ ۖ قُلْ هُوَ أَذًى ۙ فَاعْتَزِلُوا
النِّسَآءَ فِي الْمَحِيضِ ۙ وَلَا تَقْرَبُوهُنَّ حَتّٰى يَطْهُرْنَ ۚ
فَإِذَا تَطَهَّرْنَ فَأْتُوهُنَّ مِنْ حَيْثُ أَمَرَكُمُ اللهُ ۚ إِنَّ

pale Alipowaamuruni Mwenyezi Mungu; hakika Mwenyezi Mungu Huwapenda wanaotubu na wanaojitakasa.

اللّٰهَ يُحِبُّ التَّوَّابِيْنَ وَ يُحِبُّ الْمُتَطَهِّرِيْنَ ﴿٢٢٢﴾

224. Wake zenu ni shamba lenu - basi liendeeni shamba lenu wakati mpendapo, na tangulizieni (wema) nafsi zenu; na Mcheni Mwenyezi Mungu, na jueni ya kwamba bila shaka mtakutana naye; na uwapashe habari njema waaminio.

نِسَآؤُكُمْ حَرْثٌ لَّكُمْ فَاْتُوْا حَرْثَكُمْ اَنّٰى شِئْتُمْ وَ
قَدِّمُوْا لِاَنْفُسِكُمْ وَ اتَّقُوا اللّٰهَ وَ اعْلَمُوْٓا اَنَّكُمْ مُّلٰقُوْهُ
وَ بَشِّرِ الْمُؤْمِنِيْنَ ﴿٢٢٣﴾

227. Kwa wale wanaoapa kwamba watajitenga na wake zao, (muda wao) ni kungoja miezi minne; na kama wakirejea, basi hakika Mwenyezi Mungu ni Msamehevu, Mrehemevu.

لِلَّذِيْنَ يُؤْلُوْنَ مِنْ نِّسَآئِهِمْ تَرَبُّصُ اَرْبَعَةِ اَشْهُرٍ
فَاِنْ فَآءُوْ فَاِنَّ اللّٰهَ غَفُوْرٌ رَّحِيْمٌ ﴿٢٢٦﴾

229. Na wanawake waliopewa talaka wangoje mpaka hedhi tatu, wala haiwapasi kuficha Aliyoumba Mwenyezi Mungu katika matumbo yao, ikiwa wanamwamini Mwenyezi Mungu na siku ya Mwisho; na waume wao wana haki zaidi ya kuwarejesha katika muda huo, kama wakitaka isilahi. Nao (wanawake) wanayo haki sawa na ile iliyo juu yao kwa sheria; na wanaume wana daraja moja zaidi kuliko wao, na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye hekima.

وَ الْمُطَلَّقٰتُ يَتَرَبَّصْنَ بِاَنْفُسِهِنَّ ثَلٰثَةَ قُرُوْٓءٍ وَ
لَا يَحِلُّ لَهُنَّ اَنْ يَّكْتُمْنَ مَا خَلَقَ اللّٰهُ فِيْٓ اَرْحَامِهِنَّ
اِنْ كُنَّ يُؤْمِنَّ بِاللّٰهِ وَ الْيَوْمِ الْاٰخِرِ وَ بُعُوْلَتُهُنَّ اَحَقُّ
بِرَدِّهِنَّ فِيْ ذٰلِكَ اِنْ اَرَادُوْٓا اِصْلَاحًا وَ لَهُنَّ مِثْلُ
الَّذِيْ عَلَيْهِنَّ بِالْمَعْرُوْفِ وَ لِلرِّجَالِ عَلَيْهِنَّ دَرَجَةٌ
٢٨ ع ١٢
وَ اللّٰهُ عَزِيْزٌ حَكِيْمٌ ﴿٢٢٨﴾

230. Talaka (hutolewa) mara mbili; kisha ni kuwaweka kwa wema au kuwaacha kwa ihsani; wala si halali kwenu kuchukua

اَلطَّلَاقُ مَرَّتٰنِ فَاِمْسَاكٌ بِمَعْرُوْفٍ اَوْ تَسْرِيْحٌ بِاِحْسَانٍ
وَ لَا يَحِلُّ لَكُمْ اَنْ تَاْخُذُوْا مِمَّآ اٰتَيْتُمُوْهُنَّ شَيْئًا اِلَّآ

أَن يَخَافَا أَلَّا يُقِيمَا حُدُودَ اللَّهِ فَإِنْ خِفْتُمْ أَلَّا يُقِيمَا
حُدُودَ اللَّهِ فَلَا جُنَاحَ عَلَيْهِمَا فِيمَا افْتَدَتْ بِهِ تِلْكَ
حُدُودُ اللَّهِ فَلَا تَعْتَدُوهَا وَمَن يَتَعَدَّ حُدُودَ اللَّهِ
فَأُولَٰئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ ﴿٢٢٩﴾

cho chote mlichowapa (wake zenu), isipokuwa wote wawili wakiogopa ya kwamba hawataweza kusimamisha mipaka ya Mwenyezi Mungu; na kama mkiogopa kwamba hawataweza kusimamisha mipaka ya Mwenyezi Mungu, basi si aibu kwao kupokea ajikomboleacho mwanamke. Hii ndiyo mipaka ya Mwenyezi Mungu, basi msiiruke. Na atakayeiruka mipaka ya Mwenyezi Mungu, basi hao ndio wadhalimu.

فَإِن طَلَّقَهَا فَلَا تَحِلُّ لَهُ مِن بَعْدُ حَتَّىٰ تَنكِحَ زَوْجًا
غَيْرَهُ فَإِن طَلَّقَهَا فَلَا جُنَاحَ عَلَيْهِمَا أَن يَتَرَاجَعَا
إِن ظَنَّا أَن يُقِيمَا حُدُودَ اللَّهِ وَتِلْكَ حُدُودُ اللَّهِ
يُبَيِّنُهَا لِقَوْمٍ يَعْلَمُونَ ﴿٢٣٠﴾

231. Na kama amempa talaka (ya tatu), basi (mwanamke huyo) si halali kwake baada ya hayo mpaka aolewe na mume mwingine; na (mwanamume huyo) akimwacha, basi hapana aibu kwao (mume yule wa kwanza na mwanamke huyo) kurejeana ikiwa kama wana yakini ya kwamba wote wawili watasimamisha mipaka ya Mwenyezi Mungu. Na hii ni mipaka ya Mwenyezi Mungu Anayoibainisha kwa watu wajuao.

وَالَّذِينَ يُتَوَفَّوْنَ مِنكُمْ وَيَذَرُونَ أَزْوَاجًا يَتَرَبَّصْنَ
بِأَنفُسِهِنَّ أَرْبَعَةَ أَشْهُرٍ وَعَشْرًا فَإِذَا بَلَغْنَ أَجَلَهُنَّ
فَلَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ فِيمَا فَعَلْنَ فِي أَنفُسِهِنَّ بِالْمَعْرُوفِ
وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرٌ ﴿٢٣٤﴾

235. Na wale wanaofishwa miongoni mwenu na kuacha nyuma wake, hawa wangoje miezi minne na siku kumi; na wanapofikia muda wao, basi si aibu juu yenu katika yale wanayoyafanya kwa nafsi zao kwa (kufuata) sheria; na Mwenyezi Mungu Anazo habari za mnayoyatenda.

237. Si dhambi kwenu kama mkiwapa wanawake talaka ambapo hamjawagusa au kuwawekea mahari. Na wapatieni matumizi - mwenye wasaa kadiri awezavyo, na mwenye dhiki kadiri awezavyo - matumizi kwa sheria; ndio wajibu kwa wafanyao wema.

لَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ إِنْ طَلَّقْتُمُ النِّسَاءَ مَا لَمْ تَمَسُّوهُنَّ
أَوْ تَفْرِضُوا لَهُنَّ فَرِيضَةً ۚ وَمَتِّعُوهُنَّ عَلَى الْمُوسِعِ
قَدَرُهُ وَعَلَى الْمُقْتِرِ قَدَرُهُ مَتَاعًا بِالْمَعْرُوفِ ۖ حَقًّا
عَلَى الْمُحْسِنِينَ ﴿٢٣٦﴾

287. Mwenyezi Mungu Haikalifishi nafsi yo yote ila yaliyo sawa na wasaa wake; (faida ya) yale iliyoyachuma ni yake na (hasara ya) yale iliyoyachuma ni juu yake. Mola wetu, Usitushike kama tukisahau au tukikosa, Mola wetu, na Usitubebeshe mzigo kama Ulivyowabebebsha wale waliokuwa kabla yetu. Mola wetu, Usitutwike tusiyoyaweza, na Utusamehe, na Utughofirie, na Uturehemu; Wewe ndiwe mlinzi wetu; basi Utusaidie juu ya watu makafiri.

لَا يُكَلِّفُ اللَّهُ نَفْسًا إِلَّا وُسْعَهَا ۚ لَهَا مَا كَسَبَتْ وَعَلَيْهَا
مَا اكْتَسَبَتْ ۗ رَبَّنَا لَا تُؤَاخِذْنَا إِنْ نَسِينَا أَوْ أَخْطَأْنَا ۚ
رَبَّنَا وَلَا تَحْمِلْ عَلَيْنَا إِصْرًا كَمَا حَمَلْتَهُ عَلَى الَّذِينَ
مِنْ قَبْلِنَا ۚ رَبَّنَا وَلَا تُحَمِّلْنَا مَا لَا طَاقَةَ لَنَا بِهِ ۖ
وَاعْفُ عَنَّا وَاغْفِرْ لَنَا وَارْحَمْنَا ۚ أَنْتَ مَوْلَانَا
فَانْصُرْنَا عَلَى الْقَوْمِ الْكَافِرِينَ ﴿٢٨٦﴾ ع

## 4. SURA AN-NISAA

2. Enyi watu! mcheni Mola wenu ambaye Amewaumbeni kutoka katika nafsi moja, na Ameumba kutoka katika nafsi ile nafsi yenzie, , na kutoka katika nafsi hizo mbili Akaeneza wanaume wengi na wanawake; na Mcheni Yeye bilkhususi kwa kuziheshimu fungamano za kidugu; hakika Mwenyezi Mungu ni Mlinzi juu yenu.

يَا أَيُّهَا النَّاسُ اتَّقُوا رَبَّكُمُ الَّذِي خَلَقَكُمْ مِنْ نَفْسٍ
وَاحِدَةٍ وَخَلَقَ مِنْهَا زَوْجَهَا وَبَثَّ مِنْهُمَا رِجَالًا كَثِيرًا
وَنِسَاءً ۚ وَاتَّقُوا اللَّهَ الَّذِي تَسَاءَلُونَ بِهِ وَالْأَرْحَامَ ۚ
إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلَيْكُمْ رَقِيبًا ﴿١﴾

4. Na kama mkiogopa kwamba ninyi (kama jamii) mtashindwa kufanya uadilifu katika mambo yahusuyo mayatima baada ya matukio ya vita, basi oeni wanawake wa chaguo lenu wawili au watatu au wanne. Lakini mkiogopa kuwa hamwezi kufanya uadilifu, basi (oeni) mmoja tu, au wale ambao mikono yenu ya kuume imewamiliki; Hii ndiyo njia ya karibu zaidi kwa ajili yenu ili kuepukana na kutokufanya uadilifu.

وَإِنْ خِفْتُمْ أَلَّا تُقْسِطُوا فِي الْيَتَامَىٰ فَانكِحُوا مَا طَابَ
لَكُم مِّنَ النِّسَاءِ مَثْنَىٰ وَثُلَاثَ وَرُبَاعَ فَإِنْ خِفْتُمْ
أَلَّا تَعْدِلُوا فَوَاحِدَةً أَوْ مَا مَلَكَتْ أَيْمَانُكُمْ ذَٰلِكَ
أَدْنَىٰ أَلَّا تَعُولُوا ﴿٣﴾

24. Mmeharimishiwa (kuoa) mama zenu, na binti zenu, na dada zenu, na shangazi zenu, na dada za mama zenu, na binti za ndugu, na binti za dada, na mama zenu waliowanyonyesheni, na dada zenu wa kunyonya, na mama za wake zenu, na binti zenu wa kambo walio katika ulinzi wenu, waliozaliwa na wake zenu mliowaingilia - lakini kama ninyi hamjawaingilia, basi si vibaya kwenu (kuwaoa) - na wake wa wana wenu waliotoka katika migongo yenu; na (imeharimishwa) ya kwamba mwaoe madada wawili wakati mmoja, isipokuwa yale yaliyokwisha pita; hakika Mwenyezi Mungu ndiye Msamehevu, Mrehemevu.

حُرِّمَتْ عَلَيْكُمْ أُمَّهَاتُكُمْ وَبَنَاتُكُمْ وَأَخَوَاتُكُمْ وَعَمَّاتُكُمْ
وَخَالَاتُكُمْ وَبَنَاتُ الْأَخِ وَبَنَاتُ الْأُخْتِ وَأُمَّهَاتُكُمُ
اللَّاتِي أَرْضَعْنَكُمْ وَأَخَوَاتُكُم مِّنَ الرَّضَاعَةِ وَأُمَّهَاتُ
نِسَائِكُمْ وَرَبَائِبُكُمُ اللَّاتِي فِي حُجُورِكُم مِّن نِّسَائِكُمُ
اللَّاتِي دَخَلْتُم بِهِنَّ فَإِن لَّمْ تَكُونُوا دَخَلْتُم بِهِنَّ فَلَا
جُنَاحَ عَلَيْكُمْ وَحَلَائِلُ أَبْنَائِكُمُ الَّذِينَ مِنْ
أَصْلَابِكُمْ وَأَن تَجْمَعُوا بَيْنَ الْأُخْتَيْنِ إِلَّا مَا قَدْ
سَلَفَ إِنَّ اللَّهَ كَانَ غَفُورًا رَّحِيمًا ﴿٢٣﴾

وَالْمُحْصَنٰتُ مِنَ النِّسَاۗءِ اِلَّا مَا مَلَكَتْ اَيْمَانُكُمْ ۚ
كِتٰبَ اللّٰهِ عَلَيْكُمْ ۚ وَاُحِلَّ لَكُمْ مَّا وَرَاۗءَ ذٰلِكُمْ اَنْ
تَبْتَغُوْا بِاَمْوَالِكُمْ مُّحْصِنِيْنَ غَيْرَ مُسٰفِحِيْنَ ۭ فَمَا
اسْتَمْتَعْتُمْ بِهٖ مِنْهُنَّ فَاٰتُوْهُنَّ اُجُوْرَھُنَّ فَرِيْضَةً ۭ
وَلَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ فِيْمَا تَرٰضَيْتُمْ بِهٖ مِنْۢ بَعْدِ الْفَرِيْضَةِ ۭ
اِنَّ اللّٰهَ كَانَ عَلِيْمًا حَكِيْمًا ﴿٢٥﴾

25. Na pia (mmeharimishiwa) wanawake wenye kuolewa, isipokuwa wale iliyowamiliki mikono yenu ya kuume. Ndiyo sheria ya Mwenyezi Mungu juu yenu. Na mmehalalishiwa (kuoa wanawake) minghairi ya hao, kwamba mwatafute kwa mali zenu, kwa kuwaoa bila ya kufanya zinaa, Na kwa ajili ya faida mnayoipata kwao, basi wapeni mahari zao zilizolazimishwa; wala si vibaya kwenu katika yale mli yoridhiana baada ya (kutoa) mahari. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi, Mwenye hekima.

وَاِنْ خِفْتُمْ شِقَاقَ بَيْنِهِمَا فَابْعَثُوْا حَكَمًا مِّنْ
اَھْلِهٖ وَحَكَمًا مِّنْ اَھْلِھَا ۚ اِنْ يُّرِيْدَآ اِصْلَاحًا يُّوَفِّقِ
اللّٰهُ بَيْنَهُمَا ۭ اِنَّ اللّٰهَ كَانَ عَلِيْمًا خَبِيْرًا ﴿٣٦﴾

36. Na kama mkihofia uvunjaji wa ahadi ya ndoa baina yao, basi teueni mpatanishi mmoja kutoka katika jamaa za mwanamume na mpatanishi mmoja kutoka katika jamaa za mwanamke. Kama wote wawili wakitaka mapatano, Mwenyezi Mungu Atasababisha yawepo baina yao. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi, Mwenye habari.

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْٓا اَطِيْعُوا اللّٰهَ وَاَطِيْعُوا الرَّسُوْلَ وَ
اُولِي الْاَمْرِ مِنْكُمْ ۚ فَاِنْ تَنَازَعْتُمْ فِيْ شَيْءٍ فَرُدُّوْهُ
اِلَى اللّٰهِ وَالرَّسُوْلِ اِنْ كُنْتُمْ تُؤْمِنُوْنَ بِاللّٰهِ وَالْيَوْمِ
الْاٰخِرِ ۭ ذٰلِكَ خَيْرٌ وَّاَحْسَنُ تَاْوِيْلًا ﴿٦٠﴾

60. Enyi mlioamini! Mtiini Mwenyezi Mungu na Mtiini Mtume Wake na wale wenye mamlaka juu yenu; na kama mkigombana juu ya jambo lo lote, basi lirudisheni kwa Mwenyezi Mungu na Mtume, ikiwa mnamwamini Mwenyezi Mungu na siku ya Mwisho. Hiyo ndiyo heri, nayo ina matokeo bora.

## 24. SURA AN-NUUR

7. Na wale wanaowasingizia wake zao na hawana mashahidi ila nafsi zao, basi ushahidi wa mmoja wao utakuwa kushahidilia mara nne kwa kiapo cha Mwenyezi Mungu: ya kwamba bila shaka yeye ni mmoja wa wakweli.

والذين يرمون أزواجهم ولم يكن لهم شهداء
إلا أنفسهم فشهادة أحدهم أربع شهادات
بالله إنه لمن الصادقين ٦

8. Na mara ya tano (aape) kwamba laana ya Mwenyezi Mungu iwe juu yake ikiwa yu miongoni mwa waongo.

والخامسة أن لعنت الله عليه إن كان من
الكاذبين ٧

9. Na (mkewe) itamwondolea adhabu kwa kutoa ushuhuda mara nne kwa kiapo cha Mwenyezi Mungu ya kwamba huyu (mume) ni miongoni mwa waongo.

ويدرؤا عنها العذاب أن تشهد أربع شهادات
بالله إنه لمن الكاذبين ٨

10. Na mara ya tano (aape) ya kwamba hasira ya Mwenyezi Mungu iwe juu yake kama (mumewe) yu miongoni mwa wakweli.

والخامسة أن غضب الله عليها إن كان من
الصادقين ٩

31. Waambie waaminio wanaume wainamishe macho yao, na wazilinde tupu zao, hili ni takaso kwao; Bila shaka Mwenyezi Mungu Anazo habari za yale wanayoyafanya.

قل للمؤمنين يغضوا من أبصارهم ويحفظوا فروجهم
ذلك أزكى لهم إن الله خبير بما يصنعون ٣٠

32. Na waambie wanawake waami-nio kwamba wainamishe macho yao na wazilinde tupu zao, na wasidhihirishe uzuri wa sura zao wala mapambo yao isipokuwa yale yaliyo bayana katika hayo, na kwamba washushe shungi zao

وقل للمؤمنات يغضضن من أبصارهن ويحفظن
فروجهن ولا يبدين زينتهن إلا ما ظهر منها
وليضربن بخمرهن على جيوبهن ولا يبدين
زينتهن إلا لبعولتهن أو آبائهن أو آباء بعولتهن

mpaka vifuani mwao, na wasionyeshe uzuri wa sura zao wala mapambo yao isipokuwa kwa waume zao, au kwa baba zao au kwa baba za waume zao, au kaka zao au wana wa kaka zao au wana wa dada zao au wanawake wenzao au wale waliomilikiwa na mikono yao ya kuume au wale miongoni mwa watumishi wa nyumbani wa kiume ambao hawana uovu nafsini mwao, au watoto wadogo ambao hawajafikia umri wa kuwa na wazo lo lote kuhusu sehemu za siri za wanawake. Na wasitembee kwa namna ambayo inafichua uzuri waliouficha. Na tubieni nyote kwa Mwenyezi Mungu enyi waaminio, ili mpate kufaulu.

أو أبنائهن أو أبناء بعولتهن أو إخوانهن أو
بني إخوانهن أو بني أخواتهن أو نسائهن أو ما
ملكت أيمانهن أو التابعين غير أولي الإربة
من الرجال أو الطفل الذين لم يظهروا على عورات
النساء ولا يضربن بأرجلهن ليعلم ما يخفين
من زينتهن وتوبوا إلى الله جميعا أيه المؤمنون
لعلكم تفلحون ﴿٣١﴾

## 25. SURA AL-FURQAAN

55. Naye ndiye Aliyemwumba mwanadamu kwa maji, kisha Akamfanyia nasabu na ujamaa wa ndoa. Na Mola wako ni Mwenye uwezo.

وهو الذي خلق من الماء بشرا فجعله نسبا
وصهرا وكان ربك قديرا ﴿٥٤﴾

## 30. SURA AR-RUUM

22. Na katika Ishara Zake ni kuwa Amewaumbieni katika jinsi yenu wake ili mpate utulivu kwao, naye Amejaalia mapenzi na huruma baina yenu. Bila shaka katika hayo zimo Ishara kwa watu wanaofikiri.

ومن آياته أن خلق لكم من أنفسكم أزواجا
لتسكنوا إليها وجعل بينكم مودة ورحمة
إن في ذلك لآيات لقوم يتفكرون ﴿٢١﴾

## 33. SURA AL-AHZAAB

5. Mwenyezi Mungu Hakumwekea mwanadamu ye yote mioyo miwili kifuani mwake; wala Hawageuzi wake zenu kuwa mama zenu kwa sababu tu ninyi mnawaita mama zenu na mnaacha kuingiliana nao; wala Hawageuzi wale mnaowapanga uana kuwa wana wenu halisi. Hayo ni maneno ya vinywa vyenu tu; Lakini Mwenyezi Mungu Husema kweli, Naye Huongoza kwenye njia iliyo sawa.

مَا جَعَلَ اللّٰهُ لِرَجُلٍ مِّنْ قَلْبَيْنِ فِيْ جَوْفِهٖ وَمَا جَعَلَ
اَزْوَاجَكُمُ الّٰٓئِيْ تُظٰهِرُوْنَ مِنْهُنَّ اُمَّهٰتِكُمْ وَمَا جَعَلَ
اَدْعِيَآءَكُمْ اَبْنَآءَكُمْ ذٰلِكُمْ قَوْلُكُمْ بِاَفْوَاهِكُمْ وَاللّٰهُ
يَقُوْلُ الْحَقَّ وَهُوَ يَهْدِي السَّبِيْلَ ﴿٤﴾

71. Enyi mlioamini, Mwogopeni Mwenyezi Mungu na semeni usemi ulio sawa.

72. Atawatengenezeeni vizuri mwenendo wenu na Atawasameheni madhambi yenu; na anayemtii Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, bila shaka amefanikiwa mafanikio makubwa.

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوا اتَّقُوا اللّٰهَ وَقُوْلُوْا قَوْلًا سَدِيْدًا ﴿٧٠﴾
يُّصْلِحْ لَكُمْ اَعْمَالَكُمْ وَيَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوْبَكُمْ وَمَنْ
يُّطِعِ اللّٰهَ وَرَسُوْلَهٗ فَقَدْ فَازَ فَوْزًا عَظِيْمًا ﴿٧١﴾

## 58. SURA AL-MUJAADILA

4. Na wale wawaitao wake zao mama, kisha wakarudia katika yale waliyoyasema, basi wampe mtumwa uhuru kabla ya kugusana; hayo ndiyo mnaagizwa kwayo; na Mwenyezi Mungu Anajua mnayoyatenda.

وَالَّذِيْنَ يُظٰهِرُوْنَ مِنْ نِّسَآئِهِمْ ثُمَّ يَعُوْدُوْنَ
لِمَا قَالُوْا فَتَحْرِيْرُ رَقَبَةٍ مِّنْ قَبْلِ اَنْ يَّتَمَآسَّا
ذٰلِكُمْ تُوْعَظُوْنَ بِهٖ وَاللّٰهُ بِمَا تَعْمَلُوْنَ خَبِيْرٌ ﴿٣﴾

5. Na asiyepata (mtumwa) basi afunge saumu miezi miwili inayoandamana kabla ya kugusana; na asiyeweza, basi awalishe maskini sitini; (mmeambiwa) hayo ili mmwamini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake; na hiyo ni mipaka ya Mwenyezi Mungu; na kwa makafiri iko adhabu iumizayo.

فَمَن لَّمْ يَجِدْ فَصِيَامُ شَهْرَيْنِ مُتَتَابِعَيْنِ مِن
قَبْلِ أَن يَتَمَاسَّا ۖ فَمَن لَّمْ يَسْتَطِعْ فَإِطْعَامُ
سِتِّينَ مِسْكِينًا ۚ ذَٰلِكَ لِتُؤْمِنُوا بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ ۚ
وَتِلْكَ حُدُودُ اللَّهِ ۗ وَلِلْكَافِرِينَ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٥﴾

## 59. SURA AL-HASHIR

19. Enyi mlioamini! Mcheni Mwenyezi Mungu, na mtu aangalie aliyoyatanguliza kwa ajili ya kesho, na mcheni Mwenyezi Mungu; hakika Mwenyezi Mungu Anazo habari za mnayoyatenda.

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَلْتَنظُرْ نَفْسٌ مَّا قَدَّمَتْ
لِغَدٍ ۖ وَاتَّقُوا اللَّهَ ۚ إِنَّ اللَّهَ خَبِيرٌ بِمَا تَعْمَلُونَ ﴿١٩﴾

## 65. SURA AT-TALAAQ

2. Ewe Nabii! Mtakapowataliki wanawake, wapeni talaka kwa kuzinga-tia kipindi cha eda kilichowekwa, na fanyeni hesabu ya kipindi hicho cha eda; na mcheni Mwenyezi Mungu Mola wenu. Msiwatoe katika nyumba zao wala wasitoke wenyewe, mpaka wafanye jambo la ufasiki ulio wazi. Na hiyo ndiyo mipaka ya Mwenyezi Mungu; na anayeiruka mipaka ya Mwenyezi Mungu, basi hakika amejidhulumu nafsi yake. Hujui ya kwamba labda Mwenyezi Mungu Atatokeza jambo jingine baada ya haya.

يَا أَيُّهَا النَّبِيُّ إِذَا طَلَّقْتُمُ النِّسَاءَ فَطَلِّقُوهُنَّ
لِعِدَّتِهِنَّ وَأَحْصُوا الْعِدَّةَ ۖ وَاتَّقُوا اللَّهَ رَبَّكُمْ ۖ
لَا تُخْرِجُوهُنَّ مِن بُيُوتِهِنَّ وَلَا يَخْرُجْنَ إِلَّا أَن
يَأْتِينَ بِفَاحِشَةٍ مُّبَيِّنَةٍ ۚ وَتِلْكَ حُدُودُ اللَّهِ ۚ وَ
مَن يَتَعَدَّ حُدُودَ اللَّهِ فَقَدْ ظَلَمَ نَفْسَهُ ۚ لَا تَدْرِي
لَعَلَّ اللَّهَ يُحْدِثُ بَعْدَ ذَٰلِكَ أَمْرًا ﴿٢﴾

3. Basi wanapofikia muda wao, ndipo wawekeni kwa wema, au faraka-neni nao kwa wema, na mshuhudishe mashahidi wawili waadilifu miongoni mwenu, na simamisheni ushahidi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Hivyo ndivyo anaagizwa yule anayemwamini Mwenyezi Mungu na siku ya Mwisho; na anayemwogopa Mwenyezi Mungu, (Mwenyezi Mungu) Humtengenezea njia ya kuokoka,

فَإِذَا بَلَغْنَ أَجَلَهُنَّ فَأَمْسِكُوهُنَّ بِمَعْرُوفٍ أَوْ
فَارِقُوهُنَّ بِمَعْرُوفٍ وَأَشْهِدُوا ذَوَيْ عَدْلٍ
مِّنكُمْ وَأَقِيمُوا الشَّهَادَةَ لِلَّهِ ذَٰلِكُمْ يُوعَظُ بِهِ مَن
كَانَ يُؤْمِنُ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ وَمَن يَتَّقِ اللَّهَ
يَجْعَل لَّهُ مَخْرَجًا ﴿٣﴾

5. Na wale waliokoma hedhi yao miongoni mwa wanawake wenu, ikiwa mnayo shaka, basi muda wa eda yao ni miezi mitatu, na (pia ndiyo eda kwa wale) ambao hawajapata hedhi. Na wanawake wenye mimba eda yao ni mpaka watakapojitua; na anayemwogopa Mwenyezi Mungu Humfanyia mambo yake kuwa mepesi.

وَاللَّائِي يَئِسْنَ مِنَ الْمَحِيضِ مِن نِّسَائِكُمْ إِنِ ارْتَبْتُمْ
فَعِدَّتُهُنَّ ثَلَاثَةُ أَشْهُرٍ وَاللَّائِي لَمْ يَحِضْنَ وَأُولَاتُ
الْأَحْمَالِ أَجَلُهُنَّ أَن يَضَعْنَ حَمْلَهُنَّ وَمَن يَتَّقِ
اللَّهَ يَجْعَل لَّهُ مِنْ أَمْرِهِ يُسْرًا ﴿٥﴾

6. Hiyo ni amri ya Mwenyezi Mungu Aliyoiteremsha kwenu, na anayemwogopa Mwenyezi Mungu Humfutia maovu yake na Humpa ujira mkuu.

ذَٰلِكَ أَمْرُ اللَّهِ أَنزَلَهُ إِلَيْكُمْ وَمَن يَتَّقِ اللَّهَ يُكَفِّرْ
عَنْهُ سَيِّئَاتِهِ وَيُعْظِمْ لَهُ أَجْرًا ﴿٦﴾

7. Wawekeni humo humo mnamokaa ninyi, kama mpatavyo, wala msiwadhuru kwa kuwatia katika dhiki; na kama wakiwa na mimba, basi wagharimieni mpaka wao kujifungua. Na kama wakiwanyonyesheeni, basi toeni ujira wao, na shaurianeni kwa wema, na kama mkiona udhia baina yenu, basi amnyonyeshee (mwanamke) mwingine.

أَسْكِنُوهُنَّ مِنْ حَيْثُ سَكَنتُم مِّن وُجْدِكُمْ وَ
لَا تُضَارُّوهُنَّ لِتُضَيِّقُوا عَلَيْهِنَّ وَإِن كُنَّ أُولَاتِ
حَمْلٍ فَأَنفِقُوا عَلَيْهِنَّ حَتَّىٰ يَضَعْنَ حَمْلَهُنَّ فَإِنْ
أَرْضَعْنَ لَكُمْ فَآتُوهُنَّ أُجُورَهُنَّ وَأْتَمِرُوا بَيْنَكُم
بِمَعْرُوفٍ وَإِن تَعَاسَرْتُمْ فَسَتُرْضِعُ لَهُ أُخْرَىٰ ﴿٧﴾